**Waziri** Simbachawene aamuru viongozi kuwekwa mahabusu



UKURASA 3

**Watu** wanne wafa baada ya gari kutumbukia mtoni

UKURASA 3


# Nipashe

Jumatatu Machi 1, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580506

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


LIKE & FOLLOW US




**Jina la Messi latawala wagombea urais Barcelona**

UKURASA 21

# Kanuni mpya zaja kuzibana SACCOS



## YALIYOMO


UKURASA WA 5

**MANISPAA YABANWA KUREJESHA MIL. 418/-**

NIABU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline...

UKURASA WA 7

**MWALIMU MADRASA JELA UDHALILISHAJI WA MTOTO**

MWALIMU wa madrasa Kata ya Rahaleo, Manispaa ya Lindi, Ustaadhi...


## Gharama kupima corona Zanzibar zapaa

UKURASA 2



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, akiweka ngao kwenye mnara wa mashujaa wa vita vya Majimaji sehemu ambayo mashujaa 67 walinyongwa na Wajerumani mwaka 1906. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**


Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store


# Mfanyabiashara ailili TAKUKURU ‘mkopo umiza’

UKURASA 2


**MICHEZO** NGOME FC MATUMAINI KIBAO KUPANDA UK.23 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Gharama kipimo cha Corona Z'bar juu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto imetangaza gharama mpya za kipimo cha Corona kwa wasafiri wote na kila msafiri atalipia Dola 80 za Kimarekani sawa na Sh. 184,000.

Awali bei hiyo ilikuwa kwa watalii pekee kutoka nchi za Ulaya, kutoka nchi za Afrika Mashariki ilikuwa Sh. 45,000 na Watanzania ni Sh. 30,000.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Wizara ya Afya, bei hiyo itaanza kutumika leo na wasafiri wote watatakiwa kupima kwa Dola 80.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo msafiri atatakiwa kupima siku tatu kabla ya safari na utaratibu huo haotofautiani na wa awali.

Taarifa hiyo imesema kuwa vituo vitakavyotumika kwa ajili ya upimaji wa Corona ni Migombani, Lumumba, Hospitali ya Blobal, Unguja na kwa Pemba ni kituo cha Mfikiwa.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi walisema kuwa bei hiyo kwa wazawa ni kubwa hasa ikilinganishwa kipato cha Mzanzibari.

"Bei hiyo ni sawa na nusu mshahara ya kiwango cha chini hivyo tunaiomba serikali kupunguza gharama hizo," alisema Khamis Juma, mkazi wa Mjini Unguja.

Alisema ilipaswa raia kuwekewa gharama za chini za upimaji kama ilivyokuwa awali na kwamba nchi nyingine ndivyo ninazofanya kwa raia wake.

Alisema kuwa lazima serikali iwajali raia wake kwa kuwapunguzia gharama kwa sababu hiyo ni sawa na kuwakomoa na baadhi yao wanasafiri kwa kwenda masomoni, biashara na matibabu.

"Hiyo bei ni sawa na kukomoana kwa sababu hapo umeenda kupima je, ukikutwa na Corona inamaana gharama zako utarejeshewa hili jambo tunaomba serikali ilitafakari upya," alisema.

Mkurugenzi wa Kinga wa wizara hiyo, Dk. Fadhil Muhammed, alisema wamelazimika kutangaza gharama hiyo kwa wasafiri wote kutokana na kupanda kwa vipimo hivyo.

Aidha, alisema kwa msafiri ambaye atapimwa na kukutwa na virusi vya Corona, baada ya kupona hatatakiwa kutoa tena fedha kwa ajili ya kipimo na badala yake itatumika fedha ambayo ameshalipia awali.

# Kanuni mpya kuzibana SACCOS

**Na Salome Kitomari**

KANUNI za huduma ndogo za fedha inavibana vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) kwa kutaka kuwe na sera ya fedha na mikataba ya wazi yenye kutaja viwango riba kwa tarakimu badala ya asilimia.

Pia, kanuni hizo zimetoa vigezo vya leseni kuwa ni ada ya Sh. 100,000 kwa SACCOS daraja A na Sh. 300,000 kwa daraja B, na kwamba Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaweza kuagiza chama kuomba leseni ya daraja B iwapo itakidhi vigezo vya mtaji wa chini.

Kanuni hizo ni za sheria ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2018, ambayo inatoa masharti ya mtaji wa chini ni Sh. milioni 10 na wa juu ni 200 kwa SACCOS daraja la A na B.

Kwa mujibu wa kanuni ya 28 hadi 43 inataka kuwapo kwa sera ya mikopo, utaratibu wa maombi ya mikopo, ukamilishaji wa mkataba wa mikopo na mkopaji.

Mengine ni dhamana na mkopo na udhamini, vigezo vya miamala ya watu wa karibu ikiwamo masharti ya kukopesha wajumbe wa bodi, kamati ya mikopo, meneja na wanaohusiana nao.

Pia, inataka kuwapo vigezo vya miamala ya watu wa karibu ikiwamo masharti ya kukopesha wajumbe na bodi, kamati ya mikopo, meneja na wanaohusika.

Kadhalika, inataka mtaji tete usiopungua asilimia nane ya mali zote, katazo la uhamishaji wa mitaji, gawio la faida ya ziada na masharti ya kuwa na mpango wa kuongeza mtaji.

Kwa mujibu wa kanuni hizo, SACCOS zinatakiwa kuhakikisha wajumbe wa bodi wawili wana uelewa wa masuala ya fedha, uendeshaji wa biashara, uhasibu, huduma ndogo za fedha au uchumi.

Masharti mengine ni wajumbe uhakikiwa kabla ya kuanza majukumu na vigezo vya kuwaondolea sifa, uteuzi na majukumu ya kamati ya mikopo na ajira na majukumu ya meneja wa SACCOS.

Kuhusu usimamizi wa ukwasi, mali na dhima kanuni hizo zinataka kuwapo sera ya usimamizi wa mali na dhima, mpango wa dharura wa ukwasi, kiwango cha chini cha uwiano wa ukwasi na mali cha asilimia 15 ya amana za wanachama, ukomo wa amana katika benki moja wa asilimia 15 ya mtaji tete, na uwapo wa sera ya uwekezaji.

Katika hesabu na ukaguzi, vyama hivyo vinatakiwa kuwa na vitabu stahiki vya kumbukumbu za miamala, uandaaji, uwasilishaji na uwazi wa taarifa za fedha, uteuzi, majukumu na taarifa za mkaguzi wa ndani, ukaguzi wa nje na kubadilisha mkaguzi wa nje isipokuwa COASCO.

Kuhusu kumlinda mlaji, vyama hivyo vimetakiwa kuweka wazi masharti ya hisa, akiba na amana, akaunti zenye riba na masharti ya ukopeshaji, ushughulikiaji wa malalamiko ya wateja na utoaji elimu.

Masharti mengine ni mpango wa uendelezaji biashara, uwasilishaji wa taarifa za wakopaji, hatua za kiutawala, kuhama daraja la SACCOS, kipindi cha mpito na makubaliano kati ya SACCOS na waajiri.

Akifafanua, Meneja wa huduma ndogo za fedha na maduka ya kubadilisha fedha, Victor Tarimu, alisema "Unapotoa mkopo kuna uwezekano mkopo hautalipwa na kusababisha faida ya benki, SACCOS, taasisi au kampuni kupungua, na kuwa hasara ambayo wanaweza kupata iwapo mtu hatarejesha mkopo, la tengo lengo mteja akishindwa kulipa kuwe na kiwango cha fedha ilipatikana ili mtaji wa benki usiyumbe."

Alisema tengo hilo ni siku 31 hadi 90 ni kundi la angalizo asilimia 10, siku 91 hadi 180 ni chini ya kiwango tengo lake ni asilimia 30, siku 181 hadi 365 ni mashaka na tengo ni asilimia tano huku siku 365 ni hasara na tengo lake ni asilimia 100.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akihutubia katika uzinduzi wa dirisha la 'Sema na Rais Mwinyi (SNRMWINYI), kuwasilisha kero za wananchi kupitia APP hiyo na kuwafikia wahusika. Uzinduzi huo ulifanyika juzi usiku jijini Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# M/biashara ailililia TAKUKURU 'mkopo umiza' usichukue nyumba

**Na Richard Makore,** MWANZA

MFANYABIASHARA wa vyuma chakavu, Simon Chacha mkazi wa Musoma mjini mkoani Mara, ameiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kumsaidia nyumba yake isichukuliwe na mfanyabiashara aliyemkopesha 'mikopo umiza' Sh. 2,000,000 na kutakiwa kulipa Sh. milioni 14.

Akizungumza na Nipashe jana, Chacha alisema alikopa fedha hizo kwa ajili ya kupanua biashara yake ya kununua vyuma chakavu, lakini amejikuta akidaiwa Sh. milioni 14.

Alisema alikopeshwa fedha hizo na mfanyabiashara mmoja mjini Musoma kwa makubaliano ya kurejesha Sh. milioni 2.6 kwa miezi miwili.

Alisema baada ya mwezi mmoja alimpelekea mfanyabiashara huyo huyo Sh. milioni moja, na kwamba alizichukua na kusema ziwe riba na mkopo ubaki palepale. Aliongeza baada ya hapo aliomba awe analipa kidogo kidogo, lakini mfanyabiashara huyo alikataa na kung'ang'ania hati yake ya nyumba.

Aliiomba TAKUKURU kumsaidia kwa kuwa wakati anakopa fedha hizo aliweka nyumba yake kama dhamana kwa kutoa hati na kwamba hivi sasa inaweza kuuzwa.

Alisema yupo tayari kulipa kiasi alichokopa pamoja na riba, lakini ampunguzie kutoka Sh. milioni 14 hadi Sh. milioni tatu ili aweze kulipa na kuchukua hati yake.

"Kwa kweli nateseka sana, huu ni mwaka wa pili nahangaika, huyu jamaa aliyenikopesha fedha akubali kuchukua fedha zake, lakini hataki badala yake anazidi kulimbikiza riba na sasa zimefika Sh. milioni 14, kiasi ambacho siwezi kukilipa," alisema.

Aliiomba TAKUKURU kuingilia kati aweze kupata haki yake kwa sababu muda wowote nyumba ya vyumba 10 itauzwa kwa deni la Sh. milioni mbili.

TAKUKURU imekuwa msaada mkubwa kwa kusaidia wananchi wanaokopeshwa 'mikopo umiza' wakiwamo walimu na wastaafu mbalimbali.

## HABARI KITAIFA

# Simbachawene aamuru viongozi kuwekwa mahabusu

**Na Mwandishi Wetu,** KITETO

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ameamuru kukamatwa na kuwekwa mahabusu viongozi wa vijiji vya Miriongima na Kijungu, wilayani Kiteto kwa madai ya kushawishi wananchi kufanya vurugu na kuvamia eneo lililotengwa na serikali kwa shughuli za mifugo.

Viongozi hao ambao pia wapo upande wa wakulima, wanadaiwa kuchukua rushwa kwa kuuza mashamba ambayo yapo maeneo ya wafugaji na kusababisha kuibuka kwa migogoro kati ya wakulima na wafugaji katika vijiji vya Kijungu na Amei.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara na wananchi wa Kitongoji cha Miriongima, Kijiji cha Kijungu, Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara jana, Waziri Simbachawene alisema viongozi hao wa vijiji ndio wanaochochea migogoro inayoendelea kwasababu wanawadanganya wananchi na kusababisha kuvamia maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za mifugo kwa kufanya kilimo.

"Nimekuja kwasababu ya uvunjifu wa amani, nimekutana na viongozi wenu wa wilaya na mkoa, pia nimetembelea Kijiji cha Amei, na nyie hapa nimewasikiliza, kwa wale ambao mlienda kulima kule ardhi ya kijiji cha Amei, mkiamini kwamba viongozi hawa wa kijiji cha Kijungu ni wakweli, sasa muelewe kuanzia leo kwamba wamewadanganya ile ardhi sio yao kwasababu shamba hilo la jumuiya lilishakufa siku nyingi na vijiji vilishaanzishwa, mwenyekiti wa kitongoji hiki, na mwenyekiti wa kijiji hiki wanatakiwa kuchukuliwa hatua," alisema Simbachawene.

Alisisitiza kuwa haiwezekani Mwenyekiti wa Kijiji cha Kijungu kutojua kuwa kuna Kijiji cha Amei, na kilianzishwa tangu mwaka 1993 na kwamba viongozi hao ni wachonganishi na pia wameshindwa kukaa na Mwenyekiti wa Amei kuzungumza suala hilo ambalo lipo kisheria.

Aliagiza uongozi wa wilaya na mkoa, kuhakikisha viongozi wa vijiji wanaosababisha migogoro wanakamatwe na kuchukuliwa maelezo kwa kuwa imebainika migogoro mingi ndani ya Wilaya ya Kiteto ya kuuza maeneo ambayo tayari yana mipango bora ya matumizi ya ardhi katika wilaya hiyo, yanasababishwa na viongozi wa vijiji na kata.

Mkuu wa mkoa huo, Joseph Mkirikiti, alisema katika kijiji cha Amei, kuna wakulima wakubwa ambao wamewaweka wafanyakazi katika mashamba hayo, na endapo Mkuu wa mkoa pamoja na viongozi wa wilaya wakienda katika mashamba hayo, wakulima hao wakubwa hawaonekani zaidi ya wanaowafanyia kazi.

"Mheshimiwa waziri kuna watu wakubwa, hawapo zaidi ya watano, mmoja ana hekari mia tano, mwingine hekari 2000, mwingine hekari 3000, hawa watu wamelima kule, ukienda kule mashambani hukutani nao, unakutana na watendaji kazi na kuwakamata huwezi, utawaonea, na hatuwezi tatua tatizo, bado tukasisitiza hawa watu waje ofisini ili tuzungumze, lakini hawataki kuja," alisema Mkirikiti.

Mbunge wa Kiteto, Ole Lataika, alisema njia pekee ya kuluhisha tatizo hilo ni kusimamia sheria, kwasababu mkulima ni muhimu na mfugaji ni muhimu katika maendeleo.




Mkuu wa Mkoa wa Singida Dk. Rehema Nchimbi (katikati), akiongoza Kongamano la Fursa za Uwekezaji kwenye mkoa huo. Kulia ni Katibu wa CCM Mkoa wa Singida, Lucy Sheen. Kushoto ni Katibu Tawala Mkoa huo, Dk. Angelina Lutambi. **MPIGAPICHA WETU**

# Wanne wafa kwa kuzama mtoni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU wanne akiwamo Mkuu wa Chuo cha Uuguzi Lugarawa, Steven Mtega (39), wamefariki dunia kwa kuzama kwenye mto Lupali wakiwa kwenye gari waliyokuwa wakisafiria katika Kata ya lugarawa, wilayani Ludewa, mkoani Njombe.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Dk. Stanley Mlay, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya usiku watu hao walipokuwa kwenye gari aina ya Harrier wakiwa Lugarawa kwenye mapumziko.

"Walipata ajali kwenye mto Lupali, huu mto sasa hivi una maji mengi kwa sababu ya mvua zinavyonyesha, walikuwa watu wanne kwenye mambo yao ya mapumziko Lugarawa, na dereva alikuwa huyo mkuu wa chuo, wakasema wabadilishe maeneo waende Mundindi, lakini walivyofika maeneo hayo ndo wakaingia mtoni," alisema Dk. Mlay.

Dk. Mlay aliwataja wengine waliokufa kuwa Marko Mpete, fundi umeme wa Lugarawa; Merk Mwalongo (35), mjasiriamali; Rukia Mfaume (28), mhasibu wa mradi wa umeme wa Akra Lugarawa

Alisema miili iko chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospital ya Lugarawa ikisubiri taratibu za mazishi.Naye Diwani wa Lugarawa, Erasto Mhagama, akizungumza tukio hilo, alisema limelitokea mpakani kwa Kijiji cha Shaurimoyo na Kijiji cha Amani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issa, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo, na alisema wanaendelea kufuatilia.

**MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES**
P.O.BOX 429 DODOMA – TANZANIA
OFFICE LOCATION: CCM REGIONAL BUILDING ROOM No. 9
0715170553 / 0756011439

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Amri ya Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, nitauza eneo lililopo Miyuji Jiji la Dodoma mali ya IBRAHIM JUMA KASIKA lenye vipimo LRV141, LRV859, LRV845, LRV5, LRV602, LRV9, LRV603LRV843, LRV60 Ili kufidia deni analodaiwa na RASHID SEIF ABEID KILAMA. Eneo litauzwa kama lilivyo, Mnada utafanyika kwenye eneo hilo siku ya tarehe 04/03/2021 saa 11:30 asubuhi
COURT BROKER.

**MASHARTI YA MNADA KISHERIA**

- Mnunuzi atalipa asilimia 25 (25%) ya bei papo hapo na asilimia 75 (75%) atailipa ndani ya siku 14.
- Mnunuzi akishindwa kulipa asilimia 75 ndani ya siku 14, mnada utarudiwa na asilimia 25 haitarudishwa
- Mnunuzi akishanunua gharama za kubadili umiliki ni juu yake.

**MAWASILIANO simu namba**
**(+255)735/715) 170 553 COURT BROKER.**

ARIPO

**CALL FOR EXPRESSION OF INTEREST**
**CONSULTANCY FOR ORGANISATIONAL REVIEW AND JOB RECLASSIFICATION**

The African Regional Intellectual Property Organization (ARIPO) is an Intergovernmental Organization created in 1976 under the Lusaka Agreement concluded under the auspices of the United Nations Economic Commission for Africa (UNECA) and the World Intellectual Property Organization (WIPO). Membership of the organization is open to all members of the African Union (AU) or of the United Nations Economic Commission for Africa (UNECA). The present members of the Organization are: Botswana, The Gambia, Ghana, Kenya, Lesotho, Liberia, Malawi, Mauritius, Mozambique, Namibia, Rwanda, Sao Tome and Principe, Sierra Leone, Somalia, Sudan, Swaziland, Uganda, United Republic of Tanzania, Zambia and Zimbabwe. (Total: 20 Member States)

ARIPO wishes to conduct an organizational review and job reclassification exercise for the encumbered positions in the Organization as part of periodic organizational planning and review. Therefore ARIPO seeks to engage a Consultant from any part of the world to undertake organisational review and job reclassification in accordance with the International Civil Service Commission standards. The assignment shall involve benchmarking with other analogous Regional and International/Intergovernmental Organizations.

The Consultant should possess a relevant Bachelor's and Master's Degree with at least ten (10) years' proven organizational review and job reclassification experience in Intergovernmental Organizations and must not be a staff member of any of the governing bodies of ARIPO. The Consultant can be an individual or a body corporate. In the case of body corporates, the firm shall be evaluated based on the Lead Consultant's qualifications.

Interested Consultants are invited to obtain the Terms of Reference (ToRs) from ARIPO by contacting the Secretariat by email at mail@aripo.org with the reference on the subject: "Organizational Review and Job Reclassification".

Deadline: Submissions of proposals shall be by email not later than March 9, 2021. This call is not restricted to Consultants/Firms from the ARIPO Member States.

A: 11 Natal Road, Belgravia, P.O. Box 4228, Harare, Zimbabwe, T: +263 4 794 065/6/8/54/74 | +263 731 020 609, F: +263 4 794 072, E: mail@aripo.org, W: www.aripo.org

# Kunenge awatoa hofu Watanzania dawa asili

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, amewataka Watanzania kuondoa hofu ya dawa za asili zinazozalishwa nchini na kuwasisitiza wazitumie kwa kuwa zina msaada mkubwa katika kupambana na magonjwa mbalimbali ikiwamo ya upumuaji.

Aliyasema hayo juzi wakati alipotembelea Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO), lililozindua rasmi dawa aina ya COVIDOL inayoaminika kukinga maambukizi ya magonjwa mbalimbali.

"Tunatumia miti shamba yetu, lakini pia tunatumia utaalamu kutengeneza dawa hizi na zinapita kwenye vipimo maabara zinachekiwa, kwahiyo niwaambie tutumie dawa hizi tukiwa tuna uhakika ni dawa nzuri, zimetengenezwa kitaalamu, na hazina madhara," alisema Kunenge.

Kauli hiyo inakuja siku chache baada ya Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kuwataka Watanzania kutumia dawa za asili katika mapambano dhidi ya virusi vya Corona (COVID-19).

Februari 4, mwaka huu, akiwa mkoani Morogoro, Rais Magufuli alisisitiza matumizi ya miti shamba pamoja na kujifukiza kama njia za kupambana na COVID-19 na kuwa siyo kila dawa zinazotoka nje ya nchi ni nzuri kwa Watanzania. "Kuna dawa inaitwa COVIDOL, Bugiji, zinafanya kazi kwasababu zimethibitishwa na Mkemia Mkuu, kamwe msifikirie kila dawa inayotoka nje ni kwaajili yenu, ingekuwa hivyo malaria ingeisha," alisema Rais Magufuli.

Akiwa kiwandani hapo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Kunenge alilipongeza TIRDO kwa jitihada kubwa za kuendeleza viwanda vya ndani hasa kwenye utafiti na uvumbuzi wa dawa mbalimbali za asili. "Niwashukuru kwa mchango mkubwa mnaofanya katika maendeleo ya viwanda katika nchi yetu, mkoa wetu wa Dar es Salaam ni mkoa wa kibiashara na tunataka kuhakikisha tunaweka mazingira bora zaidi ya biashara kusaidia kuongeza viwanda vitakavyosaidia kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na ajira za kutosha," alisema Kunenge.

Mgunduzi wa dawa hiyo, Profesa Malebo Khamis, alisema kwa kutumia utafiti wameweza kuvumbua dawa hiyo yenye uwezo wa kupambana na matatizo ya upumuaji na mpaka sasa chupa 50,000 zinazalishwa kwa siku.

"Ujumbe wangu ni mmoja tu kwamba tunayo dawa inayofanya kazi, inayokinga na inayoponya," alisema.

# NARCO yapewa siku 7 kutoa maelezo mkataba vitalu

**Na Mbaraka Kambona,**
HANDENI

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, ameipa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), wiki moja kueleza walivyotekeleza agizo alilotoa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki la kuwachukulia hatua waliokiuka mkataba wa umiliki wa vitalu katika ranchi hizo.

Gekul alitoa agizo hilo alipokagua shughuli za Ranchi ya Mzeri iliyopo katika Halmashauri ya Mji, Handeni juzi.

Alisema kuwa Waziri Ndaki alishatoa maelekezo kwa Kampuni hiyo kuwa mpaka Februari 15 wawe wameshachukua hatua kwa walioshindwa kuendeleza vitalu walivyopangishwa ikiwamo kuwanyang'anya.

"Ndugu zangu mheshimiwa waziri alishatoa maelekezo kuhusu waliokiuka mkataba, leo ni Februari 27 (juzi), hatujapata taarifa yoyote, natoa wiki moja tupate taarifa ya utekelezaji, kauli ilishatolewa tunataka utekelezaji, vinginevyo tutaona NARCO hamtoshi," alisema Gekul.

Alisema kuwa kwa muda mrefu kumekuwa hakuna ufuatiliaji wa kina kuhusu ranchi hizo na watu kugeuza kichaka na serikali imeendelea kupoteza mapato yake.

Gekul alisema waliooneshania ya kuanza kulipa wanaweza kuvumiliwa, lakini waeleze wanampango gani na deni watamaliza lini, lakini ambao mpaka sasa hawajafanya lolote watafutwe na wachukuliwe hatua.

Pia, aliwataka NARCO kuongeza uzalishaji wa ng'ombe wa nyama na maziwa ili kukidhi mahitaji ya viwanda na kuuza nje ya nchi.

"Tunataka wawekezaji watakaofuga kibiashara katika ranchi zetu, huku hatutaki kufuga kama maonyesho, tunataka ufugaji kwenye hizi ranchi uwe wa tija ili mazao yaende yakachakatwe kwa wingi katika viwanda vyetu," alifafanua Gekul.

Alisema kuwa serikali imepunguza gharama za ukodishaji wa vitalu na sasa ni Sh. 3,500 kwa heka moja, aliwahamasisha wawekezaji ambao wana nia ya kufuga kisasa kutumia fursa hiyo kuendesha ufugaji wa kisasa katika ranchi hizo ili kuongeza tija katika uzalishaji na kuongeza pato la taifa.




Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira na mchekeshaji, Lucas Mhuvile maarufu kama Joti, wakijiandaa kupanda mti wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Tigo Green for Kili wilayani Hai jana, yenye lengo la kupanda miti 10,000 na kurejesha hadhi ya theluji ya Mlima Kilimanjaro. Kulia ni Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo. Habari Uk. 9. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wawekezaji wajadili fursa kuwekeza nchini

**Na Gwamaka Alipipi**

WAWEKEZAJI kutoka mataifa mbalimbali wamekutana jijini Dar es Salaam kujadili fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini, ikiwamo kwenye sekta ya kilimo, miundombinu na viwanda.

Kongamano hilo lilifanyika mwishoni mwa wiki na kufunguliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo.

Akizungumza wakati wa kongamano hilo, Prof. Mkumbo aliwataka wawezaji wa kigeni kuja kwa wingi kuwekeza Tanzania kwenye sekta mbalimbali kwani hakuna urasimu.

Naye Rais wa Benki ya Maendeleo Afrika, Akinwumi Adesina, alisema Tanzania inazidi kukua kwa haraka na kuongeza thamani katika uwekezaji.

Mwanzilishi wa taasisi ya Accountable Africa ambao ni waandaaji wa kongamano hilo, Thierry Dongala, alisema kongamano hilo limekuja wakati sahihi kutokana na mada mbalimbali zinazojadiliwa kuakisi maendeleo.

Mkurugezi wa taasisi ya ushauri ya MiDA Advisors, Aymeric Saha, inayotoa ushauri kwa baadhi ya taasisi kubwa kutoka Marekani zinapofanya uwekezaji katika nchi za Afrika hususani kwenye miradi ya miundombinu, alisema takribani Sh. bilioni saba zimetengwa na taasisi wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi endelevu ya miundombinu.

Baadhi ya wawekezaji walioshiriki katika mkutano huo walisisitiza juu ya serikali kuunga mkono wawekezaji kwa kuboresha mazingira. Katika kongamano hilo sekta ya kilimo ilijadiliwa zaidi kwa wawekezaji wa kigeni kuonyesha nia ya kushirikiana na wadau wadogo wa Kitanzania, ili kuongeza tija kwa lengo la kuongeza uzalishaji usiotegemea mbegu za GMO.

Mwanzilishi wa taasisi ya Reap, Peter Schuurs, alisema: "Tunatamani kuona tunaweka mtaji wetu na kufanya kazi kwa bidii kwenye ardhi ya Tanzania ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na hasa lile la kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula katika kila mkoa kwa mtindo wa uwajibikaji endelevu."

Kongamano hilo pia liliwahusisha wawekezaji wa kitanzania wanaoishi ughaibuni, kwa lengo la kuwashawishi kuwekeza nchini.

## HABARI KITAIFA

# Manispaa yabanwa kurejesha mil. 418/-

**Na Munir Shemweta,**
IRINGA

NIABU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameibana Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kurejesha Sh. milioni 418 ilizopewa na Wizara kwa ajili ya mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha viwanja katika manispaa hiyo.

Akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi na wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Iringa katika kikao kazi kilichofanyika mwishoni mwa wiki, Dk. Mabula alisema fedha ilizopewa Manispaa ya Iringa ni mkopo kwa ajili ya kupima viwanja na siyo kwa ajili ya shughuli nyingine za halmashauri.

Alisema, baada ya kukamilisha upangaji na upimaji viwanja ya Manispaa ilitakiwa kurejesha fedha ilizokopeshwa na kiasi kinachopatikana kama faida walitakiwa kuendeleza shughuli za sekta ya ardhi katika halmashauri.

"Wizara imetoa fedha ili upime viwanja na kuuza na baadaye urudishe fedha, lakini ninyi badala ya kurudisha fedha mmetumia kwenye mambo mengine, wenzenu Geita faida waliyopata katika mradi kama huu walinunua gari la idara ya ardhi, hatuwezi kutumia fedha kwa utaratibu huo," alisema Mabula.

Alizitaka halmashauri zote zilizokopeshwa fedha na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha viwanja kuzirejesha kulingana na makubaliano ili kuwezesha halmashauri nyingine zenye uhitaji kukopa.

Alisema halmashauri zitakazokaidi kuzirejesha fedha kwa wakati basi suala hilo litawasilishwa mamlaka husika ili wahusika wakatwe fedha hizo moja kwa moja.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Hamid Njovu, alimuahidi Mabula kuwa halmashauri yake itahakikisha inakamilisha kulipa deni hilo kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2020/2021.

Alisema, haikuwa nia ya halmashauri yake kutolipa deni hilo kwa wakati bali hali hiyo imesababishwa na changamoto ya malalamiko ya wananchi kutaka kuongezwa idadi ya viwanja 1,000 wakati wakiendelea na shughuli hiyo . Hata hivyo, alisema Manispaa yake inadai takriban Sh. milioni 500 kwenye mradi huo.

"Mhe Naibu Waziri wa Ardhi, naahidi kulipa deni hilo haraka iwezekanavyo na kila mwezi nitatoa milioni 50 za kulipa deni hilo" alisema Njovu.

# Wahoji ujenzi vituo vya afya kutelekezwa

**Na Daniel Limbe,** MULEBA

WAKAZI wa Wilaya ya Muleba, mkoani Kagera wameiomba serikali kukamilisha ujenzi wa majengo ya vituo vya afya ambayo yametelekezwa licha ya kutumia fedha nyingi za umma.

Kauli hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki na baadhi ya wakazi wa kijiji na kata ya Ijumbi, wilayani Muleba ambao waliitupia lawama serikali ya wilaya hiyo kushindwa kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya kwenye kata yao kwa zaidi ya miaka miwili.

Licha ya miundombinu kutokamilika kwa wakati, wananchi wamelazimika kuanza kuyatumia majengo hayo kwa huduma ya kliniki ya mama na mtoto kutokana na umbali wa kwenda hospitali ya wilaya hiyo.

Petrulida Ruhiza, mkazi wa kijiji hicho aliliambia Nipashe kuwa kutokamilika kwa kituo hicho kumesababisha wananchi kutumia fedha na muda mwingi kufuata huduma za afya makao makuu ya wilaya badala ya kuutumia kuzalisha mali.

Akijibu malalamiko hayo diwani wa kata hiyo, Wilbard Mubirigi, alikiri majengo matatu ya kituo hicho cha afya kukabidhiwa kwa halmashauri hiyo na mhisani ambaye hakupenda jina lake kutajwa gazetini, tangu mwaka 2019 kwa lengo la kutoa huduma za afya.

"Ni kweli baadhi ya miundombinu ya kutolea huduma za afya haijakamilika kwa muda mrefu japo jitihada zinafanyika ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma hizo haraka na kwa umbali unaotakiwa," alisema Mubirigi.

Kwa mujibu wa diwani huyo, bajeti ya mwaka 2020/21 na 2021/22 halmashauri hiyo imetenga Sh. milioni 50 kwaajili ya kukarabati majengo hayo pamoja na kujenga chumba cha kuchomea taka na vyoo, huku kukihitajika nyumba ya kuishi mganga mfawidhi.

Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Swalehe Mruma, alisema kutokana na jiografia ya eneo hilo, kuna haja kwa wadau wa maendeleo kusaidia ukamilishaji wa miundombinu hiyo ili kunusuru wajawazito na watoto wachanga.

Baadhi ya miradi ya maendeleo ya jamii nchini imekuwa ikiibuliwa na kutumia fedha nyingi za umma kisha kutelekezwa pasipo kukamilika kwa wakati, hali inayosababisha baadhi ya wananchi kukata tamaa ya kuchangia maendeleo.

Tpb Bank
Grow with us

PONGEZI



Hongera
**Dkt. Bashiru Ally Kakurwa** kwa kuteuliwa kuwa Balozi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
**Mhe. Dr. John Pombe Magufuli** amefanya uteuzi
Februari 26, 2021

www.tpbbank.co.tz || info@tpbbank.co.tz,
marketing@tpbbank.co.tz || facebook/tpbbank || 0787 669977

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Namungo tunataka rekodi nyingine kimataifa

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), Klabu ya Simba na Namungo, wiki hii na ijayo watashuka katika viwanja tofauti ugenini kuendelea kuipeperusha bendera ya Tanzania kimataifa.

Katika michuano hiyo, Simba inapeperusha bendera ya Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa wakati Namungo ikiwa na jukumu hilo katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, mashindano yote yakiwa na utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani humu.

Tayari wawakilishi hao wameweka rekodi kwa kuwa timu mbili za kwanza kutoka nchini kufuzu hatua ya makundi kwa msimu mmoja wa michuano hiyo ya CAF, jambo ambalo linaonyesha namna soka la Tanzania limezidi kupiga hatua.

Simba ambayo tayari imeshacheza mechi mbili za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ipo Kundi A, pamoja na AS Vita ya DR Congo, Al Ahly ya Misri, na Al-Merreikh ya Sudan. Lakini pia imeshinda mechi zake mbili za kwanza dhidi ya AS Vita ikiwa ugenini bao 1-0 na pia ikapata ushindi kama huo dhidi ya Al Ahly nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, hivyo kukaa kileleni mwa kundi hilo ikiwa na pointi sita.

Kwa upande wa Namungo, ndiyo kwanza imefuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho baada ya kuitoa Clube Desportivo Primeiro de Agosto ya Angola kwa jumla ya mabao 7-5, hivyo kupangwa Kundi D pamoja na Nkana FC ya Zambia, Pyramids ya Misri na Raja Casablaca ya Morocco.

Hivyo, wiki ijayo Machi 10, itaanzia ugenini nchini Morocco kucheza dhidi ya wenyeji wao, Raja Casablaca, ikiwa na lengo la kuendeleza moto wake ili kusaka nafasi ya kucheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza.

Lakini kwa Simba ambayo msimu wa 2018/19 wa Ligi ya Mabingwa Afrika ilifika robo fainali kabla ya kutolewa na TP Mazembe ya DR Congo, kesho inatarajia kukwea ndege kuelekea nchini Sudan tayari kwa mechi yao ya tatu dhidi ya Al-Merrikh itakayopigwa Jumamosi Machi 6.


Tayari Simba ipo katika nafasi nzuri ya kutinga robo fainali kwa mara nyingine kutokana na ushindi wa mechi zake mbili, ingawa bado kinachotakiwa kwa sasa ni kuhakikisha inashinda tena angalau mechi mbili ili kujihakikishia kwa asilimia 100 kutinga hatua hiyo.

Nipashe tunatamani kuona Simba na Namungo zikiendeleza wimbi lao la ushindi ili kuweka rekodi nyingine kwa kuwa timu za kwanza kutoka Tanzania kwa mara ya kwanza kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ndani ya msimu mmoja.

Tunatambua bado kuna milima mirefu ya kupanda kabla ya kufika hatua hiyo, lakini sisi tunaamini malengo yakiwapo huku juhudi na kujituma zikitangulizwa mbele, hakuna kinachoshindikana kwa wawakilishi hao wa Tanzania hasa kutokana na kiwango ambacho kimekuwa kikionyeshwa na wawakilishi wetu hao katika mechi zao walizocheza hadi sasa kwenye michuano hiyo ya Afrika.

Tunaamini kama mabenchi ya ufundi ya timu hizo yatakuwa yakiendeleza pale yalipoishia kutoka katika kila mchezo, kuna mwanga mkubwa kwa timu hizo kushangaza Afrika katika michuano hiyo msimu huu ambao timu nyingi zinaonekana kutokuwa fiti kutokana na kutocheza kwa muda mrefu kulikochangiwa na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona. Tunawatakia kila la kheri wawakilishi hao wa nchi katika jukumu la kuipeperusha bendera ya Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Uwekezaji unahitajika kupata zaidi ya mafanikio ya Simba, Namungo

Na Adam Fungamwango

**KWA** mara ya kwanza kwenye historia ya soka la Tanzania, timu mbili zinakwenda hatua ya makundi ya michuano mikubwa barani Afrika kwa wakati mmoja. Timu za Simba na Namungo zimetinga kwenye hatua za makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika. Ni michuano inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Simba ambayo tayari imeshatinga kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ipo kwenye Kundi A, ikiwa na timu za AS Vita ya DR Congo, Al Ahly ya Misri, na El Merreikh ya Sudan.

Kwa sasa, imeshashinda mechi mbili dhidi ya AS Vita ikiwa ugenini bao 1-0 na pia ushindi kama huo dhidi ya Al Ahly nyumbani, ikiongoza kwenye kundi lake kwa pointi sita.

Timu ya Namungo, imefanikiwa kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwa kuiondosha Clube Desportivo Primeiro de Agosto ya Angola kwa jumla ya mabao 7-5.

Timu hiyo yenye maskani yake Ruangwa mkoani Lindi, imetinga hatua hiyo na kuangukia Kundi D, ikiwa na timu za Nkana FC ya Zambia, Pyramids ya Misri na Raja Casablaca ya Morocco. Awali haikudhaniwa kama timu za Tanzania zingeweza kutinga hatua ya makundi, achilia mbali timu zote mbili kuingia kwenye hatua hiyo kwa pamoja.

Inawezekana baadhi wakaona huenda ni bahati au kuna nini kimetokea. Ukiangalia kwa jicho la tatu katika hili, utagundua kuwa timu za Tanzania kwa sasa zinaanza kupiga hatua kwenda mbele kutokana na uwekezaji kwenye soka ambao umeanza kuingia hapa nchini.

Ingawa bado kuna matatizo mengi ya kimfumo, lakini wawekezaji hawa ndiyo wanaoanza kulifanya soka la Tanzania kuanza kuheshimika nje ya nchi kwa sasa.

Tukianza kwa upande wa Simba, mwekezaji Mohamed "Mo" Dewji, amekuwa mchango mkubwa wa kupanda kwa soka la Tanzania kwa miaka michache tu hii ya karibuni, mara tu baada ya kupewa ruhusu ya kuwekeza asimilia 49 na wanachama kwenye klabu ya Simba.

Kwa misimu mitatu tu, tayari Simba imeingia hatua ya makundi mara mbili. Na hapo bado mchakato haujakamilika. Kinachofanyika ni kwamba Dewji bado anatoa ruzuku kwenye klabu hiyo ili iweze kujiendesha.

Hii ina maana Simba haijaanza kuishi kwenye uwekezaji kamili lakini kwa Namungo iliyoweka historia kutinga hatua hiyo kwa mara ya kwanza tangu ianzishwe mwaka 2016, na ikiwa ni msimu wake wa pili tu tangu ipande na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara, ni timu iliyoanzishwa na wafanyakazi wa mgodi wa Green Ganet uliopo Namungo, Kijiji cha Chingumbwa wilayani Ruangwa mkoani Lindi. Ni kwamba wawekezaji hao ndiyo wanaoibeba timu ya Namungo, na hata ilipokwenda nchini Angola, timu hiyo iliweza kukodi ndege binafsi.

Hili haliwezi kufanyika kama timu haina pesa. Tulizoea huko miaka ya nyuma timu za Tanzania zikitolewa kwenye hatua za awali tu au raundi ya kwanza ya michuano hiyo ya Afrika. Labda timu za Tanzania zipangwe na timu kutoka Comoro, Shelisheli na Madagascar ndiyo angalau zinaweza kushinda, lakini zikishapita hapo ni mara chache sana kusonga mbele.

Kwa sasa wawekezaji wamezifanya timu za Tanzania kuwa imara. Kusajili wachezaji wa gharama, wenye uwezo mkubwa na viwango vya hali ya juu vya kupambana na wapinzani wa aina yeyote. Kuwa na kambi nzuri, makocha wazuri wenye uwezo, vifaa vya mazoezi na kila aina ya vitu vinavyotakiwa kwenye soka la kisasa.

Haya yote ni gharama kubwa. Kwa maana hiyo, kinachotakiwa sasa kwa watendaji wa serikali, ni kuweka mazingira ya kuwarahisishia masharti wawekezaji ili mifumo iwe rafiki na kuwafanya wawekezaji wengine zaidi kuingia kwenye soka.

Kwa sasa klabu ya Simba ikiwa na mwekezaji wake Dewji, wanasubiri kwa muda mrefu ili uwekezaji ukamilike, lakini ni kama kumekuwa na milolongo mingi ya hapa na pale, hii inawakatisha tamaa hata wale ambao wanavizia kuwekeza kwenye klabu zingine.

Ni kwamba kwa sasa klabu za soka ambazo nazo zinaingia kwenye biashara kama kampuni, kinachotakiwa ni kanuni zake zisiwe moja kwa moja kama kampuni za kawaida, badala yake klabu za soka ambazo pia ziko kibiashara nazo ziwe na kanuni zake pekee, ambazo zitawavutia matajiri wengi kujiingiza kwenye soka kwa manufaa na soka la Tanzania.

Nina uhakika uwekezaji wa Simba ukikamilika, na wengine kama GSM nao wakafanikiwa upande wa Yanga, haitopita miaka mingi, tunaweza kuiona timu ya Tanzania ikicheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na hata kutwaa taji hilo.

HABARI KITAIFA

# Mwalimu madrasa miaka 20 jela udhalilishaji wa mtoto

**Na Said Hamdani,** LINDI

MWALIMU wa madrasa Kata ya Rahaleo,Manispaa ya Lindi, Ustaadhi Selemani Ally Mkonga (58), amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka (20) Gerezani, baada ya kupatikana na hatia ya udhalilishaji kingono mtoto mdogo mwenye umri wa miaka 12, Jina limehifadhiwa.

Licha ya kifungo pia ametakiwa kumlipa mlalamikaji (mtoto huyo) fidia ya Sh, 600,000 atakapomaliza kutumikia adhabu ya kifungo.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Lindi, Muyonga Makala, baada ya kuridhishwa pasipo shaka ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya mshitakiwa hajapewa adhabu hiyo, Hakimu Makala alimuuliza kama anazo sababu za kuishawishi ili isimpe adhabu kali kwa kosa linalomkabiri, alijitetea kwa kuomba aonewe huruma na hatarudia kosa la aina hiyo, kwani alilazimika kufanya hivyo baada ya kutingwa na Ibirisi.

Baada ya utetezi huo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Yahaya Gumbo, aliulizwa iwapo ana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu hana, lakini aliiomba Mahakama kumpa mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya aina hiyo.

Hakimu Makala akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 88/2020, kupitia kifungu 138 C (1) (a) (b) cha Sheria kanuni ya adhabu sura ya 16/2002,akasema hakubaliani na utetezi huo wa Shetani, hivyo akamuhukumu Ustaadhi Mkonga, kutumikia gerezani kifungo cha miaka 20 pamoja na kumlipa mlalamikaji fidia ya Sh. 600,000.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na Gumbo, kwamba mshtakiwa akiwa ni mwalimu wa madrasa, ambaye amekabidhiwa watoto kuwafundisha elimu ya dini, lakini amekuwa na tabia ya kuwadhalilisha watoto, akiwemo mwenye umri wa miaka (12).

Gumbo alidai kuwa mshtakiwa licha ya kuwa na umri mkubwa,,alikuwa na tabia ya kumtomasatomasa kifuani mtoto huyo bila ya ridhaa yake, hali iliyomlazimu kutoa taarifa kwa wazazi wake, na wao kuchukua hatua ya kulifikisha kituo cha Polisi.

**Kabla ya mshitakiwa hajapewa adhabu hiyo, Hakimu Makala alimuuliza kama anazo sababu za kuishawishi ili isimpe adhabu kali kwa kosa linalomkabiri, alijitetea kwa kuomba aonewe huruma na hatarudia kosa la aina hiyo, kwani alilazimika kufanya hivyo baada ya kutingwa na Ibirisi.**

# TANESCO yaokoa bil. 720/- za mitambo 12

**Na Joseph Mwendapole,** MOROGORO

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) limeokoa Sh. bilioni 720 zilizokuwa zikitumika kwa mwaka kuendesha mitambo 12 ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta kwenye mikoa mbalimbali.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Nishati, Medard Kalemani, wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa wahariri na waandishi wa habari ulioandaliwa na TANESCO.

Alisema shirika hilo lilikuwa likijiendesha kwa hasara kiasi cha kutegemea ruzuku ya zaidi ya Sh bilioni 438 kwa mwaka kutoka serikalini lakini kutokana na mipango bora ya menejmenti iliyopo sasa limeweza kujitegemea.

Alisema shirika hilo limefanikiwa kuzima mitambo 12 iliyokuwa ikizalisha umeme kwa kutumia mafuta ambayo yalikuwa mzigo mkubwa kwa shirika hilo kutokana na gharama kubwa ya ununuzi wa mafuta.

Kalemani alisema kwa miaka mitano iliyopita imekuwa ikiendelea kuimarika siku hadi siku na kundoa malalamiko yaliyokuwapo awali.

"Tumshukuru Rais Magufuli kwa kulinusuru shirika hili ambapo lilikuwa likijiendesha kwa ruzuku ya serikali ya Sh. bilioni 400 kwa mwaka, lakini tangu mwaka 2017 halipati ruzuku ya serikali na liko vizuri," alisema.

Kuhusu mradi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere, Waziri Kalemani alisema unaofadhiliwa kwa serikali kwa asilimia 100, na utakamilika kwa wakati na kwa ubora wa kimataifa.

Alisema mradi huo utagharimu fedha za ndani Sh. trilioni 6.5, na kwamba serikali inaendelea kumlipa mkandarasi wa ujenzi huo Sh. trilioni 1.9 mpaka sasa.

Waziri alisema ujenzi wa mradi huo ambao ni wanne kwa ukubwa Afrika, uko katika hatua nzuri na mkandarasi anatarajiwa kuukamilisha kwa wakati

Aidha, Waziri alisema mradi huo ni wa kwanza kwa ukubwa kwa nchi za Afrika Mashariki na ni watatu kwa ukubwa kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema kwa sasa nchi ina megawati 1,604 unaozalishwa kutokana na gesi na mji, lakini mahitaji ya sasa ni megawati 1,180 hivyo kuwa na akiba ya megawati 3,000.


Jumuiko la Maliasili Tanzania
Tanzania Natural Resource Forum

**INVITATION TO TENDER - READVERTISED**
**TENDER No. TNRF/BMZ/ 1/01/2021**

**1. Background**
The Tanzania Natural Resource Forum (TNRF) is a network organization registered in 2006 as a Non-Governmental Organization (NGO), with the aim of promoting the improvement of natural resource governance to achieve more sustainable rural livelihoods and better conservation outcomes. TNRF works for improved natural resources governance by helping to bridge the gap between:

a) People's local natural resource management needs and practices, and
b) National natural resource management priorities, policies, laws and programs

TNRF has received funding from the Federal Ministry for Economic Cooperation and Development (BMZ) through World Wide Fund for Nature (WWF) Tanzania Country Office to implement some of activities within Climate change adaptation support for community managed areas (CBNRM) project aiming at supporting Protection of key ecosystems, increased resilience and adaptation for sustainable use by local communities. Human-wildlife conflict is one of the negative impacts of climate change that not only threatens community livelihoods but also human deaths and injuries and the respective wildlife species through retaliatory attacks. Livestock are often killed or injured by wildlife species especially lions, leopards, hyenas by getting into livestock enclosures (bomas) which are usually poorly made and easily accessed by predators. Hence, constructing predator proof bomas is one secure way of reducing conflicts. TNRF therefore intends to apply part of its budgetary allocation to fund eligible payments under the contract of the project to supply materials for constructing predator proof bomas in Enduimet, Ikona, Makao and Lake

Natron WMAs to reduce human-wildlife conflicts caused by wildlife predators on livestock to communities and thus improve community livelihoods. TNRF thus intends to identify and enlist reputable and registered contractors and suppliers for:

**Lot 1;** Supply materials of for constructing 40 predator proof bomas in Enduimet WMA (20), and Lake Natron (20)
**Lot 2;** Supply materials of for constructing 40 predator proof bomas in Ikona (20) and Makao WMAs (20)

Interested suppliers/firms may purchase tendering documents from TNRF offices, Corridor Area, Arusha or via email: info@tnrf.org upon presentation of a request letter duly stating the company name and original bank slip/scanned for Tzs 100,000 (One hundred Tanzanian shillings only) for each of this service being a non-refundable fee deposited with our bank accounts details below:

**Accounts Name:** Tanzania Natural Resource Forum
**Account No:** 002 – 4002411.
**Bank Name:** Absa Bank (T) Ltd, Arusha Branch

All tenders in one original and one copy, properly filled and enclosed in plain sealed envelopes (Not indicating bidder's name) stating clearly TENDER FOR GOODS,SERVICE AND WORKS should be addressed to:

**Procurement Tender Committee**
**Tanzania Natural Resource Forum**
**P.O BOX 15605,**
**Tel: +255747158888**
**ARUSHA-Tanzania**
**TENDER No. TNRF/PRM/1/01/2021**

Deposited at the reception of Tanzania Natural Resources Forum offices, Plot # 10, Corridor
Area, Njiro, Arusha.
**Tender close on 4th March, 2021 at 1730hours**

# WMA yasimika mtambo kupima mita za umeme

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Vipimo (WMA), imesimika mtambo wa kisasa wa kupima mita za umeme kuhakikisha wananchi wanalipia kiasi sahihi cha nishati wanayotumia.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa wakala, Stela Kahwa, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe.

Naibu Waziri alitembelea kituo cha WMA Misugusugu Kibaha, Mkoa wa Pwani kuangalia maendeleo ya kituo hicho kinachopima ujazo sahihi wa matenki ya magari ya mafuta, upimaji wa mita za maji na za umeme.

Stela alimweleza Naibu Waziri kuwa kufungwa kwa mtambo huo wa kupima mita za umeme ni utekelezaji wa maagizo ya serikali kwa WMA.

"Tunashukuru kwamba tumeyatekeleza maagizo hayo yote ya serikali kwa wakati mtambo umefungwa na mita za umeme zinaanza kupimwa ili kuleta tija na thamani iliyokusudiwa na hadi Machi 15 tutaanza kupima mita hizo kwa kasi," alisema.

Naibu Waziri alielezea kufurahishwa kwake na maendeleo ya kituo hicho na kuwataka watendaji wa WMA kuendelea kukisimamia kwa kutumia weledi.

Alisema kutokana na maboresho yaliyofanyika hivi sasa magari 70 yanayosafirisha mafuta yanapimwa kwa siku hali inayowarahishia wafanyabiashara kwenda na wakati.

Kuhusu mita za maji, Naibu Waziri alisema serikali imenunua mtambo kwa kutumia Sh. milioni 500 ambapo mita zote za maji hupimwa kabla ya kufungwa.

Alisema hali hiyo imesaidia kuondoa malalamiko ya wananchi ambao wamekuwa wakilalamikia mita ambazo huwapunja maji wanapofungiwa.

# Wajawazito waondolewa adha kufuata huduma mbali

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WANANCHI wa Kijiji cha Kagezi, wilayani Kibondo wakiwamo wajawazito waliokuwa wakitembea zaidi ya kilomita 40 kufuata huduma ya upasuaji, wameondokana na adha hiyo baada ya ujenzi wa vyumba vya upasuaji na wodi ya wajawazito itakayo hudumia wananchi zaidi ya 60,000.

Wakazi hao waliishukuru uboreshaji wa huduma ya afya ya mama na mtoto katika eneo hilo uliofanywa na Shirika la World Vision Tanzania kwa ufadhili wa Serikali ya Canada kupitia mradi wa Sustain Kigoma ukijumuisha uwekaji umeme, maji, ujenzi wa vyumba vya upasuaji, wodi ya wazazi na ununuzi wa vifaa tiba muhimu ambayo wameeleza ni hatua kubwa ya kuwahakikishia usalama na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Loyce Kabi mkazi wa Kagezi alisema kabla ya uboreshwaji wa huduma katika kituo hicho wajawazito walipata adha ya kusafiri umbali mrefu, hali hiyo iliwaathiri zaidi wananchi wenye kipato kidogo wasiomudu gharama za usafiri.

Meneja wa Shirika la World Vision Mkoa wa Kigoma, Makoye Kaniki, akikabidhi rasmi majengo hayo kwa serikali ya mkoa ikiwa ni ishara ya kukabidhi vituo vingi vilivyoboreshwa katika maeneo mbalimbali mkoani humo, alisema hatua hiyo inahakikisha usalama wa masuala ya uzazi.

Naye Meneja wa mradi wa Sustain Kigoma, Doroth Sago, alisema utekelezaji wa mradi huo ulianza mwaka 2016 na ulilenga kutatua adha katika maeneo ya pembezoni ambayo ilikuwa ngumu kupata huduma ya upasuaji kutokana na kutokuwa na miundombinu ya umeme na vyumba vya upasuaji.

Alisema Sh. bilioni 2.9 zilitumika kujenga vyumba vya upasuaji, wodi za wazazi na uboreshaji wa mazingira ya kutolea huduma katika vituo vya Kagezi, Gwanumpu na Kimwanya.

Akipokea miradi hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Kamishna wa Polisi, Thobias Andengenye, alilipongeza shirika hilo kwa kuungana na serikali na kuusaidia mkoa huo kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za afya na kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Vile vile alisisitiza utunzaji wa miundombinu hiyo kwenye vituo vya afya ikiwamo kukemea tabia ya uharibifu wa vifaa hivyo kwa watumishi na wananchi wote.

"Viongozi, wananchi na watumishi wote wa umma naomba mtunze miundombinu hii pamoja na mingine ambayo imekuwa ikigharimu fedha nyingi za serikali na wahisani ili tuendelee kunufaika nayo," alisema.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud KIgahe, akipata maelezo kutoka kwa ofisa vipimo wa Wakala wa Vipimo (WMA), kuhusu mtambo wa kupima mita za umeme unavyofanyakazi katika kituo cha Misugusugu Kibaha Mkoa wa Pwani, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 24/- kupeleka maji Tinde, Shelui

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amemtaka mkandarasi ambaye anatekeleza ujenzi wa mradi wa maji ya Ziwa Victoria katika miji ya Tinde wilayani Shinyanga na Shelui wilayani Ilamba, kutumia vijana kutoka maeneo hayo wakati wa kutekeleza mradi huo.

Aweso alitoa agizo hilo katika mji mdogo wa Tinde wakati wa utiaji saini mkataba wa ujenzi wa mradi huo utakaotekelezwa na Mkandarasi Morali Mohani kutoka Kampuni ya Megha Engineering Construction ya India wenye thamani ya Sh. bilioni 24.4.

Waziri huyo alisema mradi huo ni wa miezi 12 na utahudumia wananchi wa Tinde na Shelui na kumtaka mkandarasi aumalize ndani ya muda uliopangwa huku akitumia vibarua ambao ni vijana kutoka maeneo hayo.

"Vijana ambao mtapewa vibarua kwenye utekelezaji wa mradi huu wa maji, ninawaombeni sana muwe waaminifu, msiuhujumu mradi wala kuiba vifaa vya ujenzi, bali fanyeni kazi kwa uaminifu na kujipatia kipato.

"Mradi huu ni muhimu sana kwa wananchi wa Tinde na Shelui ambao utawaondolea adha ya kufuata maji umbali mrefu na kupoteza muda wa kufanya shughuli za maendeleo," alisema.

Aweso alitoa tahadhari kwa mkandarasi kuwa huo ni mradi wake wa kwanza kutiwa saini akiwa Waziri wa Maji, hivyo hataki ubabaishaji, akisisitiza hakutakuwa na muda wa nyongeza.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Anthony Sanga, aliyetia saini mkataba huo, alisema fedha za utekelezaji wa mradi huo ni mkopo wa masharti nafuu kutoka India kupitia Benki ya Exim.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alimshukuru Rais John Magufuli kwa kutekeleza ahadi yake ya kupeleka huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Tinde na Shelui na kuahidi serikali itatoa ushirikiano kwa mkandarasi huyo ili asipate vikwazo vyovyote wakati wa utekelezaji.

# Bil. 61/- zajenga mikonga kata 1,057

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

MFUKO wa Mawasiliano kwa Wote ( USCSAF) umetumia fedha za serikali Sh. bilioni 61 kwa ajili ya kujenga mikongo katika kata 1,057 nchini .

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Uwezeshaji kutoka mfuko huo, Albert Richard ,wakati wa ukaguzi wa uzalishaji wa bidhaa za mkongo wa taifa unaofungwa katika kiwanda Cha Raddy Fidre Solution kilichopo Mkuranga, mkoani Pwani. "Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umetumia bilioni 61 za serikali kujenga mikongo kwenye kata 1,057 nchini kote, huku Mkuranga wakitumia milioni 200," alisema.

Nae Naibu Waziri wa Mawasiliano na TEHAMA, Mhandisi Kundo Mathew, alikipongeza kiwanda cha Raddy Fidre Solution kwa kuwekeza katika sekta ya mawasiliano. Akizungumza na wananchi wa Mkuranga baada ya kukagua uzalishaji wa bidhaa za mkongo wa Taifa unaofungwa na kiwanda hicho cha wazawa .

Kundo ambaye pia ni Mbunge Bariadi, alisema uwekezaji huo uliogharimu kiasi cha Sh. bilioni 1.7 utafanikisha ujenzi wa mkongo wa Taifa upungue gharama na kuokoa fedha za kigeni.

Kundo alizitaka Idara za Uhamiaji na Zimamoto kutoa ushirikiano kwa wawekezaji hao ili waweze kutimiza malengo yao .

" Idara za Uhamiaji na Zimamoto zitoe ushirikiano kwa wawekezaji hao ili waweze kutimiza malengo yao kwani kiwanda hicho kitatoa ajira zisizopungua 400, sambamba na kuongeza mapato ya Halmashauri ya Wilaya," alisema.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Ramadhani Mlanzi, alilipongeza serikali kwa kuwezeshwa kuanza ujenzi, huku akisema adhma yake ya kutengeneza kebo za fible kilomita 24000 kwa mwaka na kuongeza kuwa wao ni kati ya nchi tatu za afrika zinazofanya uzalishaji huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mhandisi Mshamu Munde, alisema mazingira rafiki kwa wawekezaji, ikiwamo ardhi ya kutosha yamewavutia zaidi ya wawekezaji 80, hali iliyochangia kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri, ikiwamo kuongezeka kwa ajira kwa vijana.



Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kalobelo (wa pili kulia), akiwa na wafanyakazi wa PPRA, walipomtembelea ofisini kwake. Wa kwanza kulia ni Meneja wa Miongozo ya Ununuzi, Castor Komba, Mtaalam wa Ununuzi, Adam Lucas (wa tatu) na David Mbangula. **MPIGAPICHA WETU**

# Mafunzo ya TANePS yalivyoinua miradi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MAFUNZO ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na Matumizi ya Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS) yanayotolewa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) yameboresha utekelezaji wa miradi katika Mkoa wa Morogoro.

Hayo yameelezwa na Katibu Tawala wa Mkoa huyo, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, alipozungumza na wawezeshaji wa mafunzo hayo kutoka PPRA waliomtembelea ofisini kwake wiki hii.

Mhandisi Kalobelo amesema kuwa ameshuhudia mabadiliko makubwa chanya katika michakato ya zabuni baada ya watendaji wa taasisi za mkoa huo kuhudhuria mafunzo hayo, hatua ambayo imesaidia kuongeza upatikanaji wa thamani ya fedha kwenye ununuzi wa umma.

"Kwakweli awali tulikuwa nyuma sana, lakini baada ya kupata mafunzo na kuanza kutumia TANePS sasa hivi tuko vizuri sana na miradi yetu mingi inaenda vizuri sana," Mhandisi Kalobelo alisema. "TANePS imepunguza gharama za makaratasi na vikao vingi. Pia, ile kuonana moja kwa moja na wazabuni kwenye hatua za mwanzo za michakato nayo ilikuwa inaongeza mianya ya rushwa na udanganyifu kwa wasio waadilifu. Lakini sasa hivi mfumo haudanganyi, wote wana fursa sawa. Na hata waki-bid wanaweka gharama ndogo ya sokoni kwakuwa hawajui nini kiko ndani ya zabuni kwenye mfumo," aliongeza.

Aidha, aliishukuru Serikali kwa kuanzisha TANePS na kutoa wito kwa taasisi nunuzi kuhakikisha watendaji wake wanashiriki kikamilifu kwenye mafunzo na kutumia elimu wanayoipata kuhakikisha kila zabuni inapitia mfumo huo kama Serikali ilivyoelekeza.

Ameishukuru pia PPRA kwa kuendelea kutoa mafunzo hayo kadri inavyowezeka, kwakuwa ukidhi wa sheria unapoongezeka miradi ya maendeleo inakamilika kwa wakati, kwa ubora unaotakiwa na kwa gharama inayoendana na mradi husika.

Naye Meneja wa Miongozo ya Ununuzi kutoka PPRA, Castor Komba, alimshukuru Katibu Tawala huyo kwa mrejesho huo na kumuomba kama mdau kuzikumbusha taasisi nunuzi zilizo chini yake kuendelea kuwawezesha watendaji kuhudhuria mafunzo hayo.

"Mamlaka inaendelea kuweka nguvu zaidi kwenye mafunzo kwakuwa ni jukumu lake muhimu lakini pia uzoefu unaonesha kadri watendaji wanavyozidi kupewa mafunzo, kiwango cha ukidhi wa sheria kinapanda angalau kila mwaka," alisema Komba.

"Hii maana yake ni kwamba watendaji wenye elimu na waadilifu wanaongeza tija kwenye jitihada za Serikali yetu ya Tanzania katika kuwaletea maendeleo wananchi kupitia miradi mikubwa na midogo inayoakisi thamani halisi ya fedha iliyotumika," aliongeza.

PPRA imefanya mafunzo ya siku nne, kuanzia Februari 23-26, 2021 mjini Morogoro, kwa watendaji takribani 50 wa taasisi mbalimbali za Serikali.

# Tigo yazindua upandaji miti 10,000 Mlima Kilimanjaro

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo, imezindua upandaji miti mkoani humo kupitia kampeni ya TIGO GREEN FOR KILI katika wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro ambapo jumla ya miti 10,000 inatarajiwa kupandwa pembezoni mwa Mlima Kilimanjaro.

Imeelezwa kuwa lengo ili kusaidia kurudisha theruji ya Mlima huo mrefu zaidi barani Afrika.

Akizungumza katika uzunduzi huo uliohudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo, alifafanua kuwa kampeni ya Tigo Green For Kili kwa ushirikiano na taasisi ya Voice of Empowered Women Foundation (VOEWOFO) ni moja ya miradi ya kujitolea ya Tigo ikiwa kama sehemu ya kurudisha kwa jamii ambayo Tigo imeshirikiana nayo kwa miaka sita mfululizo kupitia udhamini wa mbio za Tigo Kili Half Marathon zilizofanyika mjini Moshi jana.

"Tumedhamini Mbio za Tigo Kili half Marathon kwa kipichi cha miaka sita mfululizo sasa, hivyo tumeona ni vyema kurudisha kwa jamii kwa kushikiriana na taasisi ya VOEWOFO kupanda miti 10,000 itayochangia kulinda theluji ya Mlima Kilimanjaro," alifafanua Kinabo wakati wa uzinduzi huo.

Kinabo alifafanua kuwa wanatarajia kupanda miti 28,000 kabla ya mwisho wa mwaka huu, na wadau mbalimbali wamejitokeza kuchangia miti ikiwamo taasisi ya ASAS iliyochangia miti 1,000 kupitia hamasa aliyoitoa Balozi wa Tigo Green For Kili, Msanii Lucas Mvuvile maarufu kama JOTI.

"Tunatambua umuhimu wa Mkoa wa Kilimanjaro katika katika uchangiaji wa ustawi wa uchumi kwa wananchi wa mkoa huo na taifa kwa ujumla, ndio maana tumejikita kuilinda theluji ya Mlima Kilimanjaro ambayo ni kivutio kikubwa cha utalii nchini Tanzania, barani Afrika na ulimwenguni kote."

Kinabo alifafanua kuwa, kwa kutambua umuhimu wa Mkoa wa Kilimanjaro katika uchangiaji wa uchumi na ustawi wa nchi yetu kwa ujumla, Tigo wanayo furaha kushikirikiana na taasisi ya VOEWOFO kupanda miti 10,000 katika Wilaya ya Hai na siku moja kabla ya mbio ya Tigo Half Marathon 2021 na kuzindua upandaji miti huo kupitia kampeni ya Tigo Green For Kili ambapo jumla ya miti 300 imepandwa kuzunguka shule ya Msingi Mkwamakuu wilayani Hai mkoani Kilimanjaro."

Akizungumza muda mfupi kabla ya kuanza kupanda miti katika eneo la Shule ya Msingi Mkwamakuu wilayani Hai ilipozinduliwa kampeni ya Tigo Green For Kili, Mkurugenzi wa taasisi ya VOEWPOFO, Asifiwe James Mallya, aliishukuru kampuni ya Tigo kuiamini taasisi yake kutunza miti hiyo 10,000 ambayo watahusika kusimamia upandaji na utunzaje wake katika wilaya hiyo.

Pia, aliishukuru Tigo kwa ujio wake katika taasisi yake ya VOEWOFO na mradi huo wa Tigo Green For Kili kwa kuleta miti 10,000 ya kuanzia na kufafanua kuwa, zoezi hilo lina tija sana katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Hai na mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla.

Kwa upande wake, Meneja Msaidizi wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Kaskazini, Neema Mawanja, alisema kuwa taasisi yake inaunga mkono kampeni hiyo ya Tigo inayosaidia serikali katika shughuli zake za uhifadhi na usimamizi wa mazingira hasa katika misitu mbalimbali iliyotengwa, mapori ya akiba,

# TCCIA Pwani yaja kivingine

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BAADA ya kudaiwa kuyumba kwa miaka mitatu kutokana na uongozi uliokuwapo madarakani, hatimaye Taasisi ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Pwani imefanya uchaguzi, huku Said Mfinanga akiibuka mshindi wa nafasi ya mwenyekiti.

Uchaguzi huo umefanyika mwezi mmoja baada ya uongozi uliokuwapo awali kuvunjwa Januari kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yake inavyotakiwa.

Makamu mwenyekiti wa TCCIA (kilimo) ngazi ya Taifa Joseph Kaungwa, alisema uongozi wa awali ulivunjwa Januari mwaka huu, licha ya kufanya uchaguzi halali kikatiba kutokana na mambo yaliyokuwa yakifanyika.

Alisema uongozi uliopita haukuwa na ushirikiano, mahesabu hayakufanyiwa ukaguzi na kwamba viongozi wa ngazi za juu walitafakari na kuona chemba ya Pwani haiwezi kuendelea, hivyo na kuamua kuruhusu ufanyike uchaguzi na kupata viongozi ambao wataleta mabadiliko.

Alisema kiongozi ni pamoja na kuonyesha njia za mafanikio, kuunganisha wanachama na kujadili kwa pamoja mipango na namna ya kutekeleza, lakini uongozi uliopita dosari zilikuwa nyingi, hivyo mategemeo ni kuona mabadiliko sasa kwa waliochaguliwa.

Akishukuru wapigakura , baada ya uchaguzi, Mfinanga alisema atatumia elimu na uzoefu wake kuwawezesha wafanyabiashara mkoani Pwani kufanya biashara zao kwa kuweka mahesabu na kutoa mafunzo mbalimbali kuhusiana na ya masuala ya mahesabu na biashara.

Katika uchaguzi huo waligombea nafasi ya mwenyekiti walikuwa wawili akiwamo Joseph Njile aliyepata kura 20 na Mfinanga aliyeshinda kwa kupata kura 67.

# Umuhimu wanawake kuwa viongozi watajwa

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANAUME kisiwani Pemba wametakiwa kuwaunga mkono wanawake katika masuala ya uongozi, ili kutimiza malengo yao katika kuingia kwenye vyombo vya kutoa uamuzi.

Akizungumza na wananchi wa shehia ya Pandani Wilaya ya Wete, Ofisa uwezeshaji kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kwa upande wa Pemba, Asha Mussa Omar, alisema kuna mambo ambayo yanawahusu wanawake moja kwa moja, hivyo watakapoingia kwenye vyombo vya kutoa uamuzi waweze kujitetea.

Alieleza ipo haja kwa wanaume na wananchi kwa ujumla kuwashirikisha, kuwahamasisha na kuwaandaa wanawake katika misingi mizuri ili waingie katika vyombo vya kutoa uamuzi, jambo ambalo litasaidia kutetea haki zao.

"Wanawake ni waaminifu, wachapa kazi na watetezi, hivyo tunaamini kwamba watakapopata uongozi wataleta mabadiliko makubwa katika jamii, hivyo tusiwaache nyuma," alisema. Mwenyekiti wa timu hiyo, Suleiman Massoud Said, alisema wanawake ni muhimu kushiriki katika uongozi, kwani ni waathirika wakubwa, na ndio walezi wa familia, hivyo ni wasimamizi wazuri.

Isack Maganzo Nzilamoshi, kutoka Kanisa la Katoliki alisema, dini haijamkataza mwanamke kuwa kiongozi ingawa watanakiwa wasivuke mipaka ya dini yao.

Nae Sultan Khalfan Nassor alisema, wanawake wanafanya vizuri wanapokuwa viongozi, kwani wanajituma na kutatua migogoro katika jamii.

# Umbali wakwamisha 150 darasa la kwanza

**Na Christina Haule,** MOROGORO

ZAIDI ya watoto 150 wenye umri wa kuanza darasa la kwanza katika eneo la Kiegea 'B' na Ngerengere Kata ya Mkundi Manispaa ya Morogoro, wameshindwa kuanza masomo kutokana na umbali mrefu wa ilipo shule.

Watoto hao walitakiwa kutembea umbali wa kilometa 20 kwa siku kwenda shuleni, jambo ambalo lingehatarisha usalama wa maisha yao. Akizungumza wakati wa kupokea mifuko 100 ya saruji mkoani hapa, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Ngerengere, Mwajuma Mlimbo, alisema wazazi wengi wameshindwa kuwapeleka shule watoto wao kutokana na kuhofia usalama wao wakati wakienda na kurudi shule ambako ni mbali na makazi yao.

Alimshukuru Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdullaziz Abood, kwa kusaidia uanzishwaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa manne ya shule ya msingi Kiegea 'B'.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Kiegea 'B', Yohana Anthony, alisema wananchi wameshiriki kuchimba msingi, kukusanya matofali 5,000, kusomba mawe, nondo na mchanga.

Anthony alisema vifaa vingine ambavyo bado ni kokoto na ujenzi rasmi unatarajia kuanza ndani ya wiki hii ili ifikapo Juni watoto wawe wameanza kuyatumia baada ya kukamilika.

Mkazi wa Mtaa wa Kiegea 'B', Esther Petro, alisema eneo hilo wakazi wake wengi ni jamii ya wafugaji, hivyo ujio wa shule hiyo itachangia watoto wa jamii yao kupata elimu karibu na makazi yao.

"Itasaidia watoto wetu wa jamii ya wafugaji kuanza kusoma hapa kutokana na sisi kuona umuhimu wa elimu, mume wangu tumechangisha fedha za ujenzi." alisema Petro.

Petro ambaye ana watoto watano na wawili wenye umri wa kuanza shule, alisema kuwa yeye ameshindwa watoto wake kuanzishwa shule kutokana na umri wao kuwa mdogo na kutomudu kutembea umbali mrefu.

Mratibu wa ofisi ya mbunge la Morogoro Mjini, Mourice Massala, aliwapa angalizo viongozi wanaosimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa vya shule, na kuwataka wawe waaminifu na wazalendo.

"Tumejenga zahanati hapa Kiegea 'B' kwa kushirikiana na ninyi wananchi na viongozi, na mmeona ofisi ya mbunge ilivyosaidia kutoa vifaa mbalimbali... hadi leo jengo limeisha, lakini kuna kasoro zilijitokeza." alisema.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akimkabidhi hati ya umiliki wa ardhi Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu, wakati wa kikao kazi na watendaji wa sekta ya ardhi katika Mkoa wa Iringa mwishoni mwa wiki. **PICHA: MUNIRI SHEMWETA**

# Tishio la mamba laishtua serikali

**Na Gurian Adolf,** NKASI

WILAYA ya Nkasi mkoani Rukwa, imeomba kibali Wizara ya Maliasili na Utalii ili iwavune mamba ambao wamezaliana kwa wingi katika Ziwa Tanganyika na kuhatarisha maisha ya wakazi wanaoishi katika vijiji vilivyopo mwambao wa ziwa hilo.

Mkuu wa wilaya hiyo, Said Mtanda, aliyasema hayo jana alipofika katika Kituo cha Afya Nkomolo mjini Namanyere kumjulia hali kijana Thomas Kasagama (23), mkazi wa Kijiji cha Kabwe aliyenusurika kifo, baada ya kujeruhiwa na mamba.

Alisema kuwa hivi sasa kumekuwa na ongezeko kubwa la wanyama wakali kama mamba na viboko katika ziwa hilo, hali inayotishia usalama wa wavuvi na wakazi wa vijiji vilivyopo mwambao wa Ziwa Tanganyika wilayani humo.

Alisema mara kwa mara kumekuwa na matukio ya kujeruhiwa au vifo katika vijijiji hivyo, vinavyotokana na wanyama hao wakali, hali inayoonyesha lazima jitihada zifanyike ili kutokomeza hali hiyo.

"Tumelazimika kuomba kibali ili tuwavune wanyama hao, wamekuwa wengi ziwani na wamekuwa wakijeruhi na kuwaua wakazi wa vijiji vilivyopo mwambao pamoja na wavuvi, ni lazima tuwapunguze kwakua ni hatari" alisema.

Aidha, aliwataka wakazi wa vijiji hivyo kuacha tabia za kwenda kuoga, kufua nguo na kuosha vyombo pembeni ya ziwa hilo, kwa kuwa wanyama hao wanakuwa katika mawindo wakitafuta chakula, hivyo ni rahisi kuwadhuru binadamu.

Nipashe Spotika



REKODI 5 ZA SIMBA ZATETEMESHA AFRIKA UK. 12-13

# REKODI KALI 10 ZA MESSI BARCELONA




**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi ni mmoja wa wachezaji bora kabisa kwenye mchezo wa soka.

Aliwasili katika akademi ya 'La Masia' akiwa na umri wa miaka 13 na aliaanza kuichezea Barcelona mechi yake ya kwanza akiwa na miaka 17 na tangu hapo hajaangalia nyuma.

Makala haya yanaangalia rekodi 10 alizoziweka Messi tangu aanze kuichezea Barcelona katika kikosi cha kwanza mwaka 2004, twende sasa...

**#1. MATAJI MENGI - 34**

Katika kipindi chake cha uchezaji Messi ameshinda mataji 34 katika mashindano tofauti pale Barcelona. Anayefuata ni Andres Iniesta aliyeshinda mataji 32.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina ameshinda mara 10 taji la ya LaLiga, mara sita Copa Del Rey na mara nne Ligi ya Mabingwa Ullaya na Klabu Bingwa Dunia.

Msimu wa 2018-19 ndio ilikuwa mara ya mwisho kwa Barcelona kushinda taji la LaLiga, kwani msimu uliofuata walimaliza bila taji lolote.

**#9. MECHI NYINGI LALIGA - 505**

Mmoja kati ya wachezaji 12, wanne wakiwa bado wanacheza, kufikisha mechi 500 kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Huu ni msimu wake wa 17 kwenye mashindano, akifunga mabao zaidi ya 450 na kufikisha pasi za mwisho 200.

**#3. MABAO MENGI - 654**

Kwa kipindi chake cha uchezaji, Messi amefunga mabao 654 kwa Barcelona. Hakuna mchezaji aliyefikisha hata mabao 200 kwenye mashindano hayo kwa klabu.

Luis Suarez, ambaye kwa sasa anaichezea Atletico Madrid, na Cesar Rodgriguez wote wamefunga mabao 195 kwa Barcelona katika mashindano yote.

**#4. MABAO MENGI YA USHINDI KWENYE LALIGA**

Messi amefunga mabao 459 kwenye LaLiga, ambayo ni tofauti ya mabao 150 dhidi ya Cristiano Ronaldo aliyefunga 311 kwenye ligi hiyo.

Na amefunga mabao mengi zaidi katika mechi za ushindi za Barcelona yakiwa ni 121 kwenye Ligi.

**#5. MABAO MENGI LIGI YA MABINGWA ULAYA - 119**

Akiwa na mabao 119 kwenye mashindano hayo (hatua ya makundi hadi fainali), Messi anashika nafasi ya pili katika orodha ya wachezaji waliofunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, nyota huyo wa Argentina amefunga mabao mengi zaidi kama mchezaji binafsi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa klabu hiyo.

#6. Mabao mengi kwa msimu mmoja - 73 (2011-12)

Kipindi cha msimu wa kumbukumbu nzuri wa 2011-12, Messi alifunga mabao 73 kwenye mashindano yote na kuvunja rekodi ya Gerd Muller kwa kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja.

Msimu uliopita Messi alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 50 kwenye LaLiga. Alifunga mabao 14 kwenye Ligi ya Mabingwa na tisa kwenye mashindano manne tofauti.

Hata hivyo, licha ya mabao hayo ya Messi, Barcelona walimaliza nafasi ya pili nyuma ya Real Madrid kwenye LaLiga.

**#7. MABAO MENGI UEFA KWA TIMU TOFAUTI - 36**

Messi amezifunga timu 36 tofauti kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Napoli ilikuwa timu ya 36 kufungwa na Messi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Straika wa Juventus, Cristiano Ronaldo yeye amefunga dhidi ya timu 33 tofauti kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#8. MFUNGAJI WA WAKATI WOTE WA EL CLASICO**

Messi amefunga mabao 26 kwenye mchezo wa El Clasico, unaoikutanisha Real Madrid na Barcelona. Mabao 18 kati ya hayo ameyafunga kwenye mechi za Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kati ya klabu hizo. Hivyo, Messi kuwa ndio mchezaji anayeongoza kufunga kwenye El Clasico katika mechi za LaLiga.

**#9. PASI NYINGI ZA MWISHO LALIGA KWA MSIMU**

Msimu wa 2019-20, Messi alivunja rekodi ya Xavi Hernandez ya pasi za mwisho 20 kwa msimu mmoja.


**#10. KUFIKISHA TARAKIMU MBILI ZA MABAO KWENYE LALIGA MISIMU 15 MFULULIZO**

Licha ya kuanza msimu kwa kusuasu baada ya kutaka kuondoka kipindi cha majira ya joto kilichopita, Messi anaongoza kwa mabao 16 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, msimu huu.

Ni mara ya 15 mfululizo, nahodha huyo wa Argentina kufunga mabao 10 au zaidi kwenye LaLiga.

## ISIKUPITE

USHINDI alioupata Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, dhidi ya West Ham United kwenye Ligi Kuu England juzi, ni wa 500 kwa kocha huyo wa zamani wa Barcelona na Bayern Munich tangu aanze kazi ya ukocha. Lakini pia ni ushindi wake wa 200 kama kocha wa Man City katika mechi 273 - ikiwa ni michezo michache zaidi kuweza kufikiwa na kocha yeyote England kwa ushindi huo.



# KLABU 10 ZENYE MATAJI MENGI ZAIDI KARNE YA 21



Wachezaji, makocha na viongozi wa Klabu ya Al Ahly ya Misri, wakisherekea baada ya kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: MTANDAO**

**LONDON,** England

KATIKA mpira wa miguu, mataji ndio kipimo cha mafanikio kwa timu yoyote duniani.

Makocha wanatumia mbinu nyingi za ufundishaji kuhakikisha wanashinda katika kila mchezo ili kupata mafanikio ya kutwaa mataji.

**Kwa mantiki hiyo, makala haya yanakuchambulia klabu 10 zenye mataji mengi zaidi kwa karne ya 21, hizi hapa...**

### #10. AUCKLAND CITY FC (NEW ZEALAND) – MATAJI 33

Ilianzishwa mwaka 2004, Auckland City tayari imeshinda mataji nane kwenye Ligi Kuu ya ASB, mashindano makubwa zaidi ya soka nchini New Zealand.

'Navy Blues' hao ni washindi mara nane wa Kombe la OFC. Wameshinda pia taji la ASB Charity mara tano pamoja na Ligi ya Vijana.

Auckland City FC ina thamani ya euro milioni 4.35, huku mshambuliaji Emiliano Tado mwenye umri wa miaka 32, ndiye mchezaji wao ghali zaidi (Euro 450,000).

### #9. SHERIFF TIRASPOL (MOLDOVA) – MATAJI 33

Iliundwa mwaka 1997, Sheriff Tiraspol ni timu changa. Hata hivyo, tayari imepata mafanikio makubwa kwa kipindi cha miongo miwili na nusu.

Ni mabingwa wenye rekodi nchini Moldova wakishinda mataji ya ligi 18 karne hii huku pia ikishinda mara tisa taji la Moldova.

Sheriff Tiraspol ina thamani ya euro milioni 9.08. Mchezaji na nahodha wao, Veaceslav Posmac mwenye umri wa miaka 30, ndiye mchezaji ghali zaidi (Euro 700,000).

### #8. DINAMO ZAGREB (CROATIA) – MATAJI 33

Ilianzishwa mwaka 1945 baada ya kuvunjika kwa HSK Gradanski, Dinamo Zagreb ndio timu iliyoweka rekodi ya ushindi mara 21 kwenye Ligi Daraja la Kwanza Croatia.

Mshindi wa zamani wa Ligi Daraja la Kwanza Yugoslavia (kabla ya kuvunjika kwa Yugoslavia), Dinamo Zagreb imeshinda mataji 16 tangu kuanza kwa karne hii. Pia wameshinda mara 11 Kombe la Croatia.

Timu hiyo ina thamani ya euro milioni 103.35, huku mlinzi wake wa kati mwenye umri wa miaka 19, Josko Gvardiol ndiye mchezaji ghali zaidi (Euro milioni 16). Dinamo Zagreb ilifuzu hatua ya 16-bora kwenye Ligi ya Europa msimu wa 2018-19.

### #7. CELTIC (SCOTLAND) – MATAJI 33

Celtic ni moja ya klabu yenye mafanikio makubwa zaidi nchini Scotland katika historia ya mchezo huo.

Mabingwa mara 51 wa Scotland, ikishinda mataji 15 ya ligi, tisa ya mwisho wakishinda mfululizo.

Walishinda Kombe la Ulaya msimu wa 1966-67 na wana kikosi chenye thamani ya euro milioni 99.7, huku mshambuliaji wake, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 23 ndiye mwenye thamani zaidi (Euro milioni 15).

### #6. SHAKHTAR DONETSK (UKRAINE) – MATAJI 33

Shakhtar Donetsk mabingwa mara 13 wa Ligi Kuu ya Ukraine (yote wameshinda karne hii), huku wapinzani wao wakuu Dynamo Kyiv (mara 15).

Pia wametwaa mara 11 Kombe la Ukraine na mara nane Ukraine Super Cup na washindi wa Ligi ya Europa msimu wa 2008-09.

Shakhtar Donetsk kikosi chake kina thamani ya euro milioni 158.7, huku winga Tete mwenye umri wa miaka 21 ndio mchezaji ghali zaidi (Euro milioni 20).

### #5. PORTO (URENO) – MATAJI 33

Porto imekuwa ikitawala zaidi soka la Ureno tangu kuanza kwa karne hii, ikishinda mara 11 taji la Ligi Kuu katika mataji yao 29.

Dragons hao wameshinda mara nane taji la Taca de na mara 11 Supertaca Candidod.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, kwa mara ya kwanza walipata ushindi dhidi ya mabingwa wa Italia, Juventus, walipowachapa 2-1 kwenye mchezo wa kwanza hatua ya 16.

Porto pia ina kikosi chenye thamani ya euro milioni 262, na kiungo wake, Jesus Corona mwenye umri wa miaka 28 ndiye mchezaji ghali zaidi (Euro milioni 30).

### #4. BARCELONA (HISPANIA) – MATAJI 34

Barcelona ni moja ya timu kubwa sana Ulaya. Imeshinda taji la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, mara 10 na mara nne Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu kuanza kwa karne hii.

Lionel Messi na Barcelona walifurahia mafanikio makubwa zaidi chini ya kocha Pep Guardiola kati ya mwaka 2008 na 2011. Miamba hao wa Catalunya walishinda mataji sita ya nyumbani na moja la Klabu Bingwa Dunia kwa kipindi hicho.

Licha ya safu yao ya ushambuliaji kuongozwa na Messi, Barcelona kwa mara ya kwanza kwa zaidi ya muongo mmoja, walimaliza msimu uliopita bila kutwaa taji. Hawajawa kwenye kiwango kizuri chini ya kocha mpya, Ronald Koeman msimu huu, wakipitwa pointi tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu wakiwa nafasi ya tatu nyuma ya Atletico Madrid na Real Madrid.

Barcelona ni moja ya kikosi chenye wachezaji wenye thamani kubwa zaidi (Euro milioni 806), huku Lionel Messi na kinda Ansu Fati (Euro milioni 80) ndio wachezaji wenye thamani kubwa zaidi.

### #3. LINCOLN RED IMPS (GIBRALTAR) – MATAJI 40

Wana rekodi ya kushinda mara 14 mfululizo taji la Ligi Kuu ya nchini Gibraltar, ikiwa timu iliyoshinda taji la ligi mfululizo mara nyingi zaidi Ulaya.

Iliundwa mwaka 1976, na walishinda taji la Ligi Kuu Gibraltar kila mwaka kuanzia mwaka 2013 hadi 2016. Pia wameshinda taji la Rock mara 11 pamoja na Kombe la Pepe Reyes.

Kikosi chake kina thamani ya euro 825,000, huku beki wake, Scot Wiseman ndiye mchezaji ghali zaidi (Euro 200,000).

### #2. BAYERN MUNICH (UJERUMANI) – MATAJI 40

Msimu uliopita ilifikia rekodi ya Barcelona ya kushinda mataji matatu likiwamo la Klabu Bingwa Dunia kwa msimu mmoja.

Bayern Munich imeshinda mara 15 taji la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, tangu kuanza kwa karne hii. Mataji ya Bayern ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu, mara 11 Kombe la DFB Pokal, mara mbili UEFA Super Cup na mara mbili Klabu Bingwa Dunia.

Bayern Munich kikosi chake kina thamani ya euro milioni 829, huku kiungo wake, Joshua Kimmich mwenye umri wa miaka 26 akiwa ndiye mchezaji ghali zaidi (Euro milioni 90).

Mfungaji wao bora, Robert Lewandowski anashika nafasi ya tano kwenye orodha ya wachezaji ghali zaidi duniani (Euro milioni 60).

### #1. AL AHLY CAIRO (MISRI) – MATAJI 41

Ikiwa na mataji 41 na ndio klabu yenye mafanikio zaidi nchini Misri kwa karne ya 21. Mabingwa wenye rekodi ya kushinda mara 42 taji la Ligi Kuu Misri, imeshinda mara 14 taji la Ligi, mara sita taji la Misi, mara 11 Kombe la Super na mara saba Ligi ya Mabingwa Afrika tangu mwaka 2000.

Al Ahly iliifunga Palmeiras na kushinda medali ya shaba kwenye Klabu Bingwa Dunia, ikitoka kufungwa na Bayern Munich kwenye nusu fainali.

Al Ahly ina kikosi chenye thamai ya euro milioni 25.5, huku golikipa wake na nahodha, Mohamed El Shenawy mwenye umri wa miaka 32 ndio mchezaji ghali zaidi katika kikosi hicho (Euro milioni 2.5).

## Nukuu


"Bado yupo vizuri na anaweza kufanya mambo mengi ndani ya uwanja, hivyo wakati unakuja ambapo ataweza kufunga na kutupa matokeo mazuri. Namuamini kwa kuwa amekuwa akitengeneza nafasi na anatumia nafasi ndani ya uwanja, hivyo naamini ataendelea kufunga zaidi," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta akimzungumzia mshambuliaji wake, Pierre Aubameyang.**



"Nimeamua mwenyewe kufanya kitu fulani kipya baada ya msimu huu, nitaondoka klabuni na haukuwa uamuzi rahisi, ilikuwa ni ngumu sana kwa sababu nimekuwa hapa kwa miaka 13 na naitambua vizuri sana klabu hii, ipo moyoni mwangu na najivunia kucheza hapa. Bado sijaamua klabu gani nitakwenda. Hilo litatokea hapo baadaye," **Beki wa Bayern Munich, David Alaba**



"Tuna fedha nyingi za kununua wachezaji wa ajabu," alitania. "Muda wote tunashinda kwa fedha, hii ni ukweli. Na bila ya wachezaji wazuri wenye ubora, hatuwezi kufanya hivyo. Katika kundi hili kuna wachezaji bora na wanauhusiano mzuri wa kucheza pamoja na kushinda mchezo," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola**






# REKODI 5 ZA SIMBA ZATETEMESHA AFRIKA

Mfungaji wa bao pekee Simba, Luis Miquissone, akiwagonganisha mabeki wa Al Ahly ya Misri baada ya kuwachambua, kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa Jumanne iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Temeke mkoani Dar es Salaam na Simba kushinda 1-0. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa bao 1-0 ambao wawakilishi wa Afrika kwenye Ligi ya Mabingwa wameoupata Jumanne iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, umeifanya timu ya Simba kuendeleza rekodi zake safi kwenye michuano hiyo na kuitia doa Al Ahly ambayo mara ya mwisho kupoteza mechi katika mashindano hayo ilikuwa mwaka 2019.

**Mabingwa hao watetezi wa Afrika, waliduwazwa kwa kupachikwa bao lililofungwa na Luis Miquissone raia wa Msumbiji na kuondoka vichwa chini.**

Kipigo ambacho Simba imekitoa dhidi ya washindi hao wa tatu wa Kombe la Klabu Dunia, kumeifanya timu ya Simba kuweka rekodi kadhaa.

**#1. SIMBA KIBOKO YA WAARABU BONGO**

Simba imeendelea kuweka rekodi ya kuzifunga klabu zote za kutoka Afrika Kaskazini, maarufu kama 'Waarabu', kwenye ardhi ya Tanzania. Hakuna timu yoyote ile kutoka huko ambayo imecheza na Simba ikashinda Tanzania.

Timu za Waarabu ambazo zilishuka kwenye ardhi ya Tanzania na kushindwa kutoka na ushindi ni Mehala El Kubra, ilichapwa bao 1-0 mwaka 1974, Al Ahly ikabamizwa mabao 2-1 mwaka 1985, bao 1-0 mwaka 2019 na bao 1-0 Jumanne iliyopita mwaka huu. Arab Contractor ambayo kwa sasa inajulikana kama Mokawloon ikachapwa mabao 3-0 mwaka 1996, Ismailia ilifungwa bao 1-0 mwaka 2001, na mwaka 2003 Ismailia ikalazimisha suluhu na Zamalek ikafa bao 1-0 mwaka 2003.

Mwaka 2010, Simba iliiadhibu El Hahoud mabao 2-1, na ikatoka sare 2-2 dhidi ya Al Masry mwaka 2018.

Timu za Waarabu kutoka nje ya Misri ni USM Al Harach ya Algeria iliyofungwa mabao 3-0 mwaka 1993 na ES Setif mwaka 2012, iliyofungwa 2-0.

**#2. SIMBA HAIJAFUNGWA TANGU 2013**

Ni mwaka wa saba Simba haijapoteza mechi yoyote ya kimataifa ikicheza kwenye ardhi ya Tanzania.

Mara ya mwisho Simba kupoteza mechi ya kimataifa kwenye ardhi ya nyumbani ni miaka saba iliyopita. Ilikuwa ni Februari 17, 2013 ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Recreativo do Libolo ya Angola, ikiwa ni Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Baada ya hapo, timu hiyo imekuwa ikishinda au kutoka sare tu. Sare ya mwisho ilikuwa ni Aprili 6, 2019, ilipotoka suluhu bila kufungana dhidi ya TP Mazembe, mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**#3. YAVUNJA REKODI YA AL AHLY AFRIKA**

Kipigo hicho kimevunja rekodi ya Al Ahly ambayo ilikuwa haijapoteza mechi yoyote ya Ligi ya Mabingwa Afrika tangu mwaka juzi.

Mara ya mwisho Al Ahly kupoteza ilikuwa ni Novemba 29, 2019, ilipochapwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Etoile du Sahel ya Tunisia. Ilikuwa ni mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, kabla ya Simba kutibua rekodi hiyo.

**#4. YAVUNJA REKODI YA MIEZI MITANO**

Al Ahly ilikuwa haijafungwa mechi yoyote kwenye ardhi ya Afrika kwa miezi mitano sasa. Achilia mbali mechi ambayo ilifungwa mabao 2-0 dhidi ya Bayern Munich ya Ujerumani nje ya bara la Afrika, ilikuwa haijapoteza ikiwa Afrika kwa miezi mitano.

Mara ya mwisho kupoteza ilikuwa ni kwenye Ligi Kuu nchini Misri, Agosti 20, mwaka jana ilipochapwa mabao 3-1 na mahasimu wao wakubwa Zamalek.

**#5. YAMTIA DOA MOSIMANE**

Simba imeweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza ya Afrika kuifunga Al Ahly chini ya kocha Pitso Mosimane ambaye alijiunga na timu hiyo akitokea Mamelodi Sundowns.

Tangu kocha huyo ajiunge na timu hiyo Septemba 30, mwaka jana, alikuwa hajafungwa na timu yoyote ile Afrika, zaidi ya kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Bayern Munich ya Ujerumani, hivyo kumtia doa kwa kumharibia rekodi yake safi aliyokuwa nayo.

**JE, WAJUA?**



STRAIKA Michail Antonio, amekuwa mchezaji wa kwanza West Ham kufunga bao nyumbani na ugenini dhidi ya Manchester City, kwenye msimu wa Ligi Kuu tangu Iain Dowie alipofanya hivyo msimu wa 1995-96. Mchezaji huyo alifunga bao hilo juzi wakati wakichezea kichapo cha mabao 2-1 ugenini.





# JKT yaomba maabara kupima udongo

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limeiomba Wizara ya Kilimo kujenga maabara ya kisasa ya kupima afya ya udongo na kutoa majibu kwa wakati ili wananchi walime mazao kulingana na aina ya udongo uliopo kwenye maeneo yao.

Akizungumza mwishoni mwa wiki baada ya kusaini mkataba wa ushirikiano baina ya wizara hiyo na JKT wa kukuza sekta ya kilimo, Kaimu Mkuu wa Tawi la Utawala na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo Mkakati wa JKT, Kanali Hassan Mabena, alisema moja ya kikwazo kwenye kilimo ni ukosefu wa maabara kubwa ya kisasa ambayo itasaidia kuainisha aina ya udongo.

Kanali Mabena alisema wananchi wengi hawana elimu ya afya ya udongo, maabara hiyo ikijengwa itasaidia wakulima kupata mazao mengi na kujua aina ya yanayostahili kupandwa kwenye eneo hilo. "Unakuta sehemu ambayo mkulima alitakiwa kupata magunia 10 za mahindi kwa heka moja, lakini kutokana na kutokujua afya ya udongo badala ya kupanda mahindi katika eneo husika anapanda karanga, matokeo yake hupata hasara," alisema Kanali Mabena.

Hata hivyo, alisema maabara zilizopo zinachelewesha majibu huku akiomba wizara hiyo ikilisimamia hilo kwa karibu haitawakwamisha wakulima kuendesha kilimo kulingana na aina ya udongo uliopo.

Aliomba suala hilo liangaliwe kwa karibu na kulifanyia kazi, ili maabara hiyo ipatikane.

Kuhusu pembejeo za kilimo, alisema jeshi hilo lilinunua matrekta 15 na zana nyingine kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo. Kanali Mabena alisema utekelezaji wa jeshi hilo umelenga kuzalisha mazao ambayo yatajitosheleza kwa chakula na wananchi kwa ujumla.

Kwa upande wake, Katibu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alilihakikishia jeshi hilo kuwa baadhi ya kero zinazowakabili watashirikiana na kuzitatua ili kuhakikisha kilimo kinakuwa na tija.

Alisema mipango iliyopo ni kupima udongo kwa halmashauri zote nchini na watalipatia jeshi kifaa hicho ili kisaidie kujua aina za udongo katika maeneo mbalimbali wanayofanya kilimo.

"Natoa upendeleo kwa JKT ya kuwapa kifaa hicho kwa ajili ya kupima aina ya udongo katika maeneo ambayo wanafanya shughuli za Kilimo," alisema.

Alipongeza JKT katika shughuli zake za kilimo na kuahidi kuendelea kushirikiana na jeshi hilo ili kuhakikisha kila wanachohitaji katika kilimo wanafanikisha.



Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk.Suleiman Serera (kushoto), akizungumza na ujumbe wa benki ya NMB Kanda ya Kati ulioongozwa na Meneja wa NMB Kanda ya Kati , Nsolo Mlozi (kulia), walipotembelea wilaya hiyo juzi kutoa misaada mbalimbali ya kijamii. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Chigongwe waondokana adha ya maji chumvi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKAZI wa Kata ya Chigongwe jijini hapa, wameondokana na adha ya kutumia maji yenye chumvi kali baada ya kuchimbiwa kisima chenye uwezo wa kuhudumia wananchi zaidi ya 10,000.

Kisima hicho ni cha 11 kati ya 20, vilivyoahidiwa na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu 2020 na kuahidi vitachimbwa kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo ya pembezoni ili wananchi waondokane na tatizo la maji.

Akizindua kisima hicho jana, Mavunde alisema wakati wa kampeni hizo alitoa ahadi ya kuchimba visima 20 ndani ya mwaka mmoja baada ya kuchaguliwa kwenye nafasi hiyo na anaendelea kuchimba vilivyosalia ili kutekeleza hilo.

"Nashukuru Taasisi ya Dar-Ul-Muslimeen kwa ufadhili wa kisima hiki ambao umefikia sasa visima 11 ambavyo vinaendelea kuchimbwa na vingine vilivyokamilika ndani ya jimbo hili," alisema.

Pia alishukuru serikali kwa kukubali kugharamia usimikaji mabomba makubwa ili kusambaza maji kwa urahisi kwa wananchi wote wa Chingongwe.

Aliwataka wananchi kutunza mradi huo kwa maslahi ya jamii ili udumu kwa muda mrefu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Muslim Bhanji, alishukuru wananchi hao kwa ushirikiano wao walioonesha wakati wa ujenzi wa mradi huo na kuahidi kuendelea kushirikiana na mbunge huyo kutatua kero mbalimbali za wananchi.

Awali, diwani wa kata hiyo, Simon Machela, alimshukuru mbunge huyo kwa kusaidia kutatua tatizo lao la kukosa majisafi na salama kutokana na waliyokuwa wakitumia yalikuwa na chumvi kali ambayo haifai kwa matumizi ya binadamu.

# Miti 6,000 ya matunda, kivuli kupandwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali ya Rafiki Wildlife Foundation Tanzania kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Mkoa wa Dodoma, linatarajia kupanda miti 6,000 ya kivuli na matunda ikiwa ni sehemu ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Mkurugenzi Mtendaji wa asasi hiyo, Mchungaji Clement Matwiga, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu kilele cha siku ya wanyamapori duniani ambayo hufanyika kila mwaka Machi 3 na mwaka huu maadhimisho yatafanyika mkoani Dodoma.

Alisema katika maadhimisho hayo, miti 6,000 ya kivuli na matunda itapandwa maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Alisema upandaji miti huo utashirikisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, viongozi mbalimbali wa madhehebu ya dini, wanafunzi wa shule za msingi, Chuo cha Decca na wadau mbalimbali.

"Rafiki Wildlife Foundation tangu kuanzishwa kwake 2015, imefanikiwa kuifikia jumla ya mikoa sita kwa ajili ya kushiriki upandaji wa miti kwa vitendo ambayo ni mikoa wa Manyara, Singida, Kilimanjaro, Tanga, Simiyu na Dodoma," alisema.

Alisema asasi hiyo pamoja na upandaji na miti, utunzaji wa mazingira pia inashiriki kupiga vita ya ujangili.

Alihamasisha Watanzania kujenga utamaduni wa kupanda miti ya kivuli na matunda na kuacha kujihusisha na uharibifu wa mazingira pamoja na viumbe hai.





## Wakusanya kodi waaswa urasimu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imezitaka Taasisi za Umma zinazotoa vibali na kukusanya kodi kwa wawekezaji, kuacha urasimu wakati wa kutoa huduma zao ili kuchochea kasi ya uwekezaji mkoani humo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alitoa wito huo juzi wakati akizindua kituo kipya cha mafuta kilichojengwa na Kampuni ya Mafuta ya Manyanya katika eneo la Kadege jijini Mbeya.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wawekezaji wanaowekeza mkoani Mbeya, kuhusu urasimu mkubwa unaofanywa na taasisi za umma ambao unawakatisha tamaa kuongeza uwekezaji na kutamani kwenda kuwekeza kwenye mikoa mingine ama nchi zingine.

Alizitaja baadhi ya taasisi zinazolalamikiwa na wawekezaji kwa vitendo vya urasimu kuwa ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Wakala wa Usalama mahali pa Kazi (OSHA) na Halmashauri za miji na Majiji.

"Nimefika hapa leo kutoa message (ujumbe) kwa taasisi zetu za umma kuacha urasimu kwa wawekezaji, tunahitaji taasisi hizi ziwe marafiki na wawekezaji kwa kuwasaidia kuwekeza au kupanua uwekezaji wao na sio kuwa maadui na kuwakwamisha," alisema Chalamila.

Alisema endapo vitendo vya urasimu kwa wawekezaji vitaendelea mkoa hautafika mbali na pia serikali itakosa kodi inayostahili kwa vile wawekezaji hao wanaweza kuhamia maeneo mengine au kupunguza uwekezaji wao na hivyo kulipa kiwango kidogo cha kodi serikalini.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo wa kituo cha mafuta, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, alisema kuwa uwapo wa wawekezaji wengi ndani ya halmashauri yake una manufaa makubwa kwa wananchi kwa vile wawekezaji hao wanalipa ushuru na kuongeza pato la halmashauri.

Alisema fedha hizo zinazolipwa na wawekezaji ndizo zinazotumika kuwapelekea wananchi huduma muhimu za kijamii kama vile ujenzi wa shule na miundombinu mingine inayohitajika kwenye jamii.

Kwa upande mwakilishi wa Kampuni ya Manyanya, Priscus Mwaya, alisema kuwa kampuni hiyo ina jumla ya vituo sita vya mafuta ndani ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya ambavyo wameviunganisha na mifumo ya yote ya tozo za serikali.

Alisema kuwa kutokana uwekezaji huo, pia wametoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa wakazi wa Jiji la Mbeya na hivyo kuongeza kipato kuanzia ngazi ya familia hadi serikalini.

Mwaya aliiomba serikali kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji ili wazidi kujitanua na kuleta manufaa kwa wakazi wa jiji la Mbeya na taifa kwa ujumla.

# Chunya yalia ushuru wa huduma

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

UONGOZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya unakusudia kwenda kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo na Waziri wa Madini, Dotto Biteko, ili kutoa uamuzi juu ya ushuru wa huduma kati ya wilaya hiyo na Songwe kutokana na shughuli za madini ya dhahabu zinazofanyika. Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, aliyasema hayo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani kilichokuwa kinajadili na kupitisha rasimu ya bajeti kwa mwaka 2021/2022.

Alisema kuna mgogoro wa ushuru wa huduma katika Wilaya hiyo na eneo la Mkwajuni lilipo Wilaya ya Songwe kuhusu uhalali wa nani anapaswa kupata kiasi kikubwa na ushuru huo.

Alidai walikwishaafikiana jambo hilo kwa uongozi wa Mkoa wa Mbeya pamoja na Songwe, lakini hadi sasa hakuna suluhu iliyopatikana.

"Tumepanga kwenda Dodoma kuonana na waziri wa TAMISEMI na Madini ili kutoa uamuzi juu ya nani anapaswa kuchukua ushuru wa huduma zitokanazo na madini, maana wenzetu wanang'ang'ania wakati tukifuata sheria... hawapati kitu, tumejitahidi kukaa meza moja ili kutumia busara walau tuwagawie asilimia kidogo, lakini hawataki," alisema Simon.

Alisema kwa busara waliyoitumia walitaka Halmshauri ya Wilaya ya Chunya ichukue asilimia 70 na wenzao wawagawiwe asilimia 30, lakini bado kiasi hicho wamekikataa wanataka sawa kwa sawa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, alisema Baraza la Madiwani ni miongoni mwa watakao kwenda kuonana na Waziri, na kwamba tayari taratibu zote za maandalizi ya safari zimekamilika.

Alisema kupitia kikao na mawaziri hao watapata mwafaka juu ya jambo hilo ambalo hadi sasa inaikosesha mapato Halmashauri.

Alisema ushuru wa huduma zitokanazo na madini pamoja na matumizi ya barabara ni maeneo muhimu ambayo yanategemewa na Wilaya hiyo katika kuongeza mapato ambayo yataongeza uchumi na kuwaletea maendeleo wananchi.

Ofisa Mipango wa Wilaya hiyo, Yaledi Mgulla, alisema miongoni katika mwaka wa fedha 2020/2021 wameshindwa kukusanya mapato kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwemo baadhi ya watu kutotimiza wajibu wao katika ukusanyaji wa ushuru.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Wilaya, Mayeka Simon, aliwaomba madiwani kuhamasisha ukusanyaji wa mapato kwa kuongeza ufuatiliaji bila kujali hali ya maambukizi ya Virusi vya Corona.




Mkuu wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, akichukua vipimo wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Afya kwa wafanyakazi wa Benki ya CRDB ambao wanaendesha programu ya Ustawi wa Jamii kwa kuzingatia utoaji wa elimu ya saikolojia, afya ya akili na kubadili mtindo wa maisha ili kutimiza majukumu yao jana . **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Watakiwa kujenga utamaduni wa kujifukiza

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATANZANIA wamehamasishwa kujenga utamaduni wa kujifukiza ili kujikinga na janga la corona pamoja na magonjwa mengine ya kuambukiza.

Mtaalam na tabibu wa dawa za asili mkoani Mbeya, Joshua Lawrence, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na Nipashe juu ya umuhimu wa kujifukiza kama njia ya kupambana na corona.

Alisema utamaduni wa watu kujifukiza unafanywa na mataifa mbalimbali duniani, hivyo wananchi wasipuuze kwani watajikinga na magonjwa mbalimbali.

"Kujifukiza ni njia nzuri ya kukabiliana na corona nchi mbalimbali duniani zinafanya hivyo... nawahamasisha wananchi kufanya hivyo kwani ni njia salama haina madhara kama wengine wanavyodai," lisema Tabibu Lawrence.

Kuhusu mahitaji ya kujifukiza, Lawrence alisema mtu anaweza kufanya kulingana na mazingira aliyopo kwa kutumia mimea kama mkaratusi, lakini hata maji pekee huku likitumika taulo safi au blanketi na dakika 10 hadi 15 zinatumika.

Aliongeza kuwa njia ya kujifukiza ina joto lenye sentigredi 75 huku joto la mwilini likiwa na zaidi ya sentigredi 30, hivyo njia hiyo inaongeza kinga ya mwili katika kupambana na magonjwa ya mfumo wa hewa na mengine.

Alisema katika kitabu chake alichokichapisha kinaeleza faida 10 za kujifukiza katika kupambana na corona kimesheheni elimu na njia nzuri zitakazowasaidia watanzania.

Baadhi ya wananchi mkoani Mbeya, wamepongeza jitihada zilizofanywa na Tabibu hiyo katika kukabiliana na corona, na kwamba watakitafuta kitabu hicho ili kupata maarifa ya kujifukiza.

Amos Mwakilema, alisema njia za asili zina msaada mkubwa katika kujikinga na magonjwa mbalimbali na kwamba wazee wa zamani walikuwa wakizitumia.



# Mwinyi aagiza mradi wa ZUSP kukamilika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametembelea baadhi ya maeneo ya mradi wa Huduma za Jamii Mijini (ZUSP) huku akitoa agizo la kuhakikisha hadi mwisho wa Mei sehemu ambazo hazijakamilika katika eneo la Barabara ya uwanja wa Ndege wa Zanzibar hadi Mnazimmoja ziwe zimekamilika.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake hiyo, ambayo alipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali yaliyomo kwenye mradi wa ZUSP katika Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na kukagua jaa kuu la kuhifadhia taka huko Kibele.

Akizungumza baada ya ziara yake aliyotembea kwa miguu kutoa Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume hadi Mnazimmoja, alieleza kuridhishwa na maelekezo aliyoyatoa wakati wa ziara yake kama hiyo ya Disemba 9, mwaka jana licha ya kuwa baadhi ya maeneo hayajakamilika na kutaka hadi mwisho wa mwezi huu yakamilike. Alisema kwamba barabara hiyo kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Karume hadi Mnazimmoja ndio iwe kigezo kwa barabara zingine zote za mji wa Zanzibar na kinachoonekana ni kuwa bado barabara nyingi za mji ni chafu.

Alisema atazivunja manipsaa zote zilizokuwapo Mjini kama hazifanyi kazi na haiwezekani kuwapo kwao wakati mji ni mchafu.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alisikitishwa na tabia ya maeneo ya hifadhi ya barabara kufanywa sehemu ya biashara na kuagiza kutafutwa taratibu za kuhakikisha kadhia hiyo inaondoshwa.

Pia, alieleza jinsi ya miti iliyopandwa katika barabara za mjini pamoja na kuwapo baadhi ya taa ambazo haziwaki na kutoa agizo kwa wale wote waliopewa jukumu hilo katika mradi wa ZUSP kuhakikisha tatizo hilo linafanyiwa kazi.

Hivyo, aliutaka uongozi wa Serikali ya Mkoa, Wilaya na Manispaa katika kuhakikisha suala la usafi na mipango ya miji linafanyiwa kazi, huku akisisitiza umhimu wa kukusanya kodi na kuwataka Wakurugenzi wa Manispaa kuhakikisha wanakusanya kodi. Katika ziara hiyo, Rais Dk. Mwinyi aliitaka Wizara ya Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara kuhakikisha inalitengeneza vizuri eneo la barabara iliyokaa muda mrefu bila ya kutiwa lami na kuleta usumbufu kwa wapita njia.

Dk. Mwinyi pia alitembelea eneo la Maruhubi katika kituo cha kukusanya taka ambapo hajaridhishwa na kituo hicho kutokana na bado hakijafanya kazi yake ipasavyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana, alieleza jitihada zilizochukuliwa katika kuzuia uchimbaji mchanga katika eneo la Kwarara pamoja na utupaji taka ovyo kwa kushirikiana na ulinzi shirikishi ambapo wamezikamata gari sita zilizokua zikichota mchanga.




Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu (wa nne kushoto), akiwasilisha mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (AMF), Asma Mwinyi (wa tatu kulia), kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi na ukarabati wa vyoo vya Shule ya Awali, Msingi na Sekondari ya Kandwi iliyoko Unguja, Zanzibar. Wanaoshuhudia ni Meneja Mwandamizi wa benki hiyo Zanzibar, Mwinyimkuu Ngalima (wa tatu kushoto), maofisa wa benki hiyo pamoja na wawakilishi wa shule hiyo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# SMZ yahimiza kilimo cha viungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imewataka wakulima kujikita kulima mazao ya viungo (SPICES) na matunda ambayo soko lake katika nchi za nje lipo la uhakika.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na maendeleo ya Viwanda, Dk. Islam Seif, wakati akizindua kamati ya ushauri ya utekelezaji wa mradi wa mazao ya viungo na kuwashirikisha wakurugenzi wa taasisi husika na sekta binafsi. Dk. Seif alisema ujio wa mradi wa viungo ni mkombozi kwa wakulima vijijini ambao utasaidia kupata kipato kikubwa na hivyo kumudu kuendesha familia na kupambana na umasikini.

Alisema visiwa vya Zanzibar katika miaka ya 1950 hadi 1985 kilikuwa maarufu na kuongoza kwa uzalishaji na usafirisha nje ya nchi mazao ya viungo.

Aidha alisema mradi huo utakua suluhisho la kutatua tatizo la ajira katika kilimo cha viungo na utasaidia kukidhi ahadi ya Rais ya kutoa ajira 300,000.

"Tatizo kubwa la bidhaa zetu kukosa viwango hivyo ni vyema kuhakikisha bidhaa zetu ninakua na kiwango," alisema.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina matarajio makubwa kupitia mradi huo, na kwamba utekelezaji wake utaisaidia ikiwamo kuwaletea maendeleo ya wananchi sambamba na kukuza ajira.

Alieleza kuwa kwa muda mrefu wakulima wa Zanzibar wamekua wakikabiliwa na changamoto mbali za uzalishaji wa mazao bora ambayo huwapelekea kukosa soko la kimataifa.

"Kwa mkakati huu wa mradi ni wazi kuwa sasa wakulima wengi Zanzibar wataondokana na shida ya masoko ya bidhaa zao badala yake watakwenda kuziona fursa mpya za kilimo ambazo zitawaingizia kipato kikubwa," aliongeza.

Hata hivyo, Dk Islam, alisema Serikali imedhamiria kukuza pia bidhaa za wajasiriamali wa ndani pamoja na kutengeneza mazingira ya viwanda vidogo pamoja na kuzipa hadhi bidhaa zinazotengenezwa na wanachi wenyewe.

Kwa upande wake, Meneja mkuu wa mradi huo wa viungo kanda ya Unguja Amina Ussi Khamis, alisema mradi huo utatoa fursa kwa wakulima wapatao 21,000 kutoka takribani shehia 50 za Unguja na Pemba.

Alieleza kuwa kilimo kitakachohusika ni mboga matunda na viungo kama mdalasini, hiliki, tangawizi, vanila, pilipilimanga sambamba na kuongeza thamani ya mazao yanayotokana na wakulima.

Pamoja na hayo alieleza kuwa mradi huo pia utafungua fursa za masoko ya kimataifa kwa bidhaa zinazolimwa na wakulima kutoka visiwani Zanzibar kupitia mkakati maalumu ambao utaanzishwa na kuratibiwa vyema.

## Exim yasaidia mil. 10/- ujenzi vyoo shuleni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya Exim imetoa Sh.milioni 10 kwa taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (AMF) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi na ukarabati wa vyoo vya Shule ya Awali, Msingi na Sekondari ya Kandwi iliyoko Unguja, Zanzibar.

Hatua hiyo ni sehemu ya dhamira endelevu ya benki hiyo katika kusaidia sekta za elimu na afya nchini.

Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu, aliwasilisha msaada huo kwa Asma Mwinyi, Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi AMF katika hafla ya makabidhiano ambayo ilifanyika katika viwanja vya shule hiyo .

"Tumejitolea kuhudumia watu, biashara na jamii kwa ujumla. Benki ya Exim na AMF kwa pamoja tuna dhamira inayofanana ya kusaidia juhudi za kielimu na ustawi wa wanafunzi wetu na shule kote nchini. Wanafunzi hutumia muda mwingi zaidi katika siku wakiwa shuleni hivyo ni muhimu zaidi tukiweka jitihada katika kuboresha mazingira ya vyoo vyao," alisema.

"Tunafurahi kuwa sehemu ya mkakati huu muhimu unaolenga kuinua mazingira ya elimu Zanzibar. Tunaona kwamba taasisi ya AMF kuwa mshirika sahihi katika kufanikisha dhamira hiyo. Benki ya Exim tumekuwa wadau wakubwa katika kusaidia sekta ya elimu katika jamii yetu, na tunatarajia kupanua juhudi hizo hapa Zanzibar," aliongeza.

Ikiwa ni taasisi isiyojiendesha kibiashara yenye makao yake nchini, AMF imejikita zaidi katika kukuza programu ambazo zinaboresha maendeleo ya jamii katika mazingira ya vijijini na mijini, kushughulika haswa na wasichana na wanawake wenye mahitaji ya elimu, afya, na mahitaji mengine ya msingi katika jamii zao.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya AMF, Asma Mwinyi, aliishukuru benki ya Exim huku akibainisha kuwa msaada huo utagusa maisha ya wanafunzi wengi kwa miaka mingi ijayo.

"Wadau wetu muhimu na washirika kama Benki ya Exim ndio nguzo muhimu kwa mafanikio yetu. Tunashukuru kwa msaada huu ambao utasaidia katika kukarabati vyoo vya Shule ya awali, Msingi na Sekondari ya Kandwi," alibainisha.

Kulingana na taarifa ya wasemaji wa shule hizo, Kheir Juma Pandu na Juma Haji Ame, kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa vyoo hivyo kutasaidia kuhudumia wanafunzi zaidi 700 waliopo katika shule hiyo.

"Tunatumai kuwa ukarabati huu utasaidia watoto kuzingatia kwa zaidi masomo yao," walieleza.

Wlitoa wito kwa taasisi zingine za kifedha na wadau wanaopenda kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya kujifunzia katika shule za umma nchini kujitokeza kwa wingi katika jitihada.

# Misitu, nyuki zatajwa fursa kukuza uchumi

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa sekta ya misitu na nyuki, wameazimia kuongeza kasi ya matumizi ya mazao hayo kwa kuhakikisha yanakuwa chanzo muhimu cha kukuza uchumi wa nchi kupitia uwekezaji wa viwanda na uboreshaji zaidi katika tafiti.

Wamesema ili kufanikisha hilo, ni lazima kuweka nguvu zaidi katika kuboresha mnyororo wa thamani katika mazao misitu na nyuki.

Maazimio hayo yalifikiwa juzi wakati wa kufunga kongamano la Kimataifa la Sayansi juu ya mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na nyuki kwa maisha endelevu na uchumi wa viwanda.

Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya kongamano hilo, Dk. Sima Bakengesa, alisema wamebaini kutokuwapo kwa matumizi sahihi ya mazao ya misitu na nyuki yaliyoboreshwa pamoja na kwamba sekta hiyo ni muhimu katika kuongeza mapato na kukuza uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja.

Pia alisema wadau wa sekta hiyo walipendekeza misitu yote ilindwe kuanzia ngazi ya kata, kuhamasisha matumizi mbadala ya mkaa zaidi ikiwamo kuwa kwa mwongozo wa matumizi endelevu ya mbao.

Kadhalika, walishauri kuwapo kwa takwimu sahihi ambazo zitawekwa kielektroniki, kuwapo kwa njia sahihi ya kurasimisha rasilimali hiyo ya misitu na nyuki, mfumo bora wa kusambaza taarifa za mazao hayo na kutaka tafiti zifanyike zaidi kuhusu nishati mbadala.

Akifunga kongamano hilo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mkuu wa Idara ya Misitu na Nyuki katika wizara hiyo, Dk. Ezekiel Mwakalukwa, alisema serikali itafanyia kazi mapendekezo hayo kupitia mpango wa tatu wa Taifa wa Utafiti wa Misitu wa mwaka 2021-2031 na mpango wa kwanza wa Taifa wa Utafiti wa Nyuki wa mwaka 2020-2030.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), ambao ndio waandaaji wa kongamano hilo, Dk. Revocatus Mushumbusi, alisema kongamano hilo limekuwa na tija kwa nchi na kimataifa kwa sababu lilishirikisha wanasayansi kutoka Tanzania, Kenya, Sudan na Finland.

## PM akoshwa na msaada wa Coca-Cola

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya vinywaji baridi ya Coca-Cola Kwanza imetoa msaada wa madawati 100 kwa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha sekta ya elimu katika maeneo ya vijijini.

Akipokea msaada huo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema mchango huo umekuja kwa wakati mwafaka katika kipindi cha kuanza mwaka mpya wa masomo.

Majaliwa alisema msaada huo wa madawati kutoka Coca-Cola Kwanza unaonyesha uhusiano mzuri uliopo baina ya serikali na sekta binafsi ambayo inanufaisha jamii.

"Msaada huu wa madawati kutoka kwa Coca-Cola Kwanza umekuja kwa wakati mwafaka wakati ambapo tunashuhudia idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiandikisha kuanza masomo kutokana na elimu bure inayotolewa na serikali,"alisema Majaliwa.

"Kwa sababu hiyo, ni jukumu letu kila mmoja kuhakikisha kuwa madawati haya yanatunzwa vizuri kwa manufaa ya wanafunzi waliopo kwa sasa na hata kwa wale ambao watajiunga na shule kwa siku za usoni."

Mkurugenzi wa masuala ya Umma na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Salum Nassor, alisema madawati hayo yana thamani ya Sh.milioni 10. Alisema lengo lake kuu ni kuinua sekta ya elimu katika maeneo ya yaliyopo pembezoni pamoja na kutatua changamoto za uhaba wa madawati kwenye shule za msingi.

Pia, alisema wanafanya hivyo kuonyesha shukrani yao na kurudisha kwa jamii faida wanayoipata.

"Lengo la Coca- Cola Kwanza ni kuboresha maisha ya Watanzania katika sekta mbalimbali ikiwamo elimu, na hii ni moja ya sababu ya kutoa madawati haya kwa Wilaya ya Ruangwa," alisema.




Fundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) akirekebisha bomba la inchi 8 linalotoa maji kwenye tanki la Changanyikeni na kusambaza kwa wananchi wa maeneo Kibululu mpaka Goba jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Mvomero yapigwa jeki huduma jamii

**Na Mwandishi Wetu,** TURIANI

WILAYA ya Mvomero mkoani Morogoro imepatiwa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 18.5 kusaidia kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii katikaWilaya ya Mvomero.

Vifaa hivyo vimetolewa na Benki ya NMB kwa ajili ya maendeleo ya elimu na kuimarisha utoaji wa huduma ya afya ni madawati yenye thamani ya Sh. milioni 10 pamoja na vifaa vya hospitali vilivyogharimu Sh. milioni 8.5.

Msaada huo ulitolewa Alhamisi iliyopita kwa shule mbili zilizopo katika tarafa ya Turiani na vituo viwili vya kutoleahuduma ya afya.

Shule ya Msingi Mkindo 'B' imesaidiwa madawati 50 na Shule ya Sekondari ya Diangoya imepewa meza 40 na viti 40 pia. Benki ya NMB imeichangia Hospitali ya Turiani magodoro nane, vitanda nane na mashuka 50, huku Kituo cha Afya Kibati kikipata mabenchi ya kukalia wagonjwa.

Baada ya kupokea misaada hiyo, Mkuu wa Wilaya yaMvomero, Albinus Mugonya, aliishukuru NMB kwa kuendelea kuchangia shughuli za maendeleo wilayanihumo.

"Benki ya NMB imekuwa mahiri kwenye kuunga mkono juhudi za maendeleo za wananchi na kuisaidia Serikali kuboresha huduma za jamii. Naguswa na jinsi mnavyoendelea kutushika mkono sisi watu wa Mvomero na tunaomba msichoke kutusaidia," alisema.

Naye Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper, aliushukuru uongozi wa wilaya kwa juhudi zake za maendeleo ya wananchi, ambao alisema ni wadau wakubwa katika mafanikio ya benki hiyo.

## Meya Dar asaidia mtoto mlemavu

**Na Maulid Mmbaga**

MEYA wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto ametimiza ahadi yake ya kukabidhi kiti mwendo (Wheelchair) kwa mtoto mwenye ulemavu, Ally Amiri, mkazi wa Mtaa wa Mfaume, Kata ya Liwiti.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo jana, alisema Amiri ambaye ana tatizo la ulemavu, amekuwa akipata shida kwa muda mrefu kwa sababu ya kutokuwa na kiti cha kutembelea.

Alisema sambamba na hilo atamkatia Amiri bima ya afya ya mwaka mzima kutokana na kuonekana kuwa anasumbuliwa na maradhi kwa muda mrefu.

Aidha meya huyo, aliahidi kumsaidia kiti mwendo Yahaya Bakari, ambaye pia ni mlemavu, baada ya kupelekwa kwake na mzazi wake, Hadija Ramadhani, baada ya mzazi huyo kusumbuka na kijana wake kwa kipindi kirefu.

## HABARI KIMATAIFA

# UNICEF yafarijika wanafunzi kuachiwa

**Abuja,** NIGERIA

MWAKILISHI wa Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) Nigeria, Peter Hawkins, kupitia taarifa iliyoitoa alisema amefarijika kupokea habari iliyokuwa ikisubiriwa kwa hamu ya kuachiliwa kwa wanafunzi.

Wanafunzi 27 wa Chuo cha Sayansi cha Serikali huko Kagara, walitekwa kutoka shuleni kwao wiki moja iliyopita.

Alisema kwamba anatarajia kurudi katika familia zao salama.

Hawkins alisema wakati wanafunzi walioachiliwa huru wanarudi kwa familia zao, anaungana na familia ya mwenzao Benjamin Habila, aliyeuawa kwa kupigwa risasi wakati wa shambulio la usiku shuleni.

**Fikra zangu na sala ziko pamoja na familia ya Benjamin, ambao wamepata hasara kubwa.**

"Fikra zangu na sala ziko pamoja na familia ya Benjamin, ambao wamepata hasara kubwa."

Aidha kiongozi huyo wa UNICEF nchini Nigeria, alisema tukio la kushambulia shule huko Kagara, kama vile lile lililotokea katika shule ya sekondari ya wasichana ya serikali Jangebe kwenye jimbo la Zamfara, hayapaswi kulengwa katika mashambulizi, hususani katika maeneo ambayo wanategemea kuwa salama, shuleni.

"Mashambulio kwenye vituo vya elimu ni ukiukaji mkubwa wa haki za watoto. Watoto hawapaswi kamwe kuwa walengwa wa shambulio na bado, mara nyingi sana nchini Nigeria wamekuwa waathirika wa mashambulio kwenye shule zao." Hawkins alisisitiza.

Taarifa yake ilisema kuwa mashambulio kama hayo si tu yanapuuza haki za watoto kupata elimu, pia hufanya watoto kuogopa kwenda shule, wazazi wanaogopa kupeleka watoto shuleni.

Hawkins alitoa wito akisema, "tunapokaribisha habari za kuachiliwa kwa wanafunzi wa Kagara waliotekwa nyara, naomba serikali iharakishe hatua juu ya kuachiliwa na kurudishwa salama kwa wanafunzi waliotekwa nyara wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Serikali Jangebe na watoto wote wa shule waliotekwa nyara ambao bado hawajaachiliwa. **UN**

## Watano akiwamo mtoto wauawa

**Hodeida,** YEMEN

OFISA mmoja wa kijeshi nchini Yemen ameliambia Shirika la Habari la AFP kwamba watu watano akiwamo mtoto mdogo wameuwawa leo jana.

Tukio hilo ni wakati nyumba yao iliporipuliwa karibu na bandari ya Bahari ya Sham mjini Hodeida, katika mapigano ya hivi karibuni ya wenyewe kwa wenyewe nchini humo.

Hata hivyo serikali ya nchi hiyo inayoungwa mkono na Saudi Arabia na waasi wa Houthi ndio wanaolaumiwa kwa shambulio hilo.

Waasi wa Houthi wanaoungwa mkono na Iran walisema mlipuko huo ulisababishwa na mashambulio mawili ya angani kutoka kwa muungano wa kijeshi unaoongozwa na Saudi Arabia.

Hodeida, eneo lililo Kusini Magharibi mwa mji uliotekwa na waasi wa Sanaa ni njia muhimu ya kupitisha chakula, mafuta na misaada ya kibinaadamu.

Mwezi Uliopita Umoja wa Mataifa ulionya maelfu ya raia wa Yemen wako katika hatari baada ya mapigano kuongezeka mjini Hodeida. **DW**

## Wanajeshi wauawa kwa shambulizi bomu

**Mogadishu,** SOMALIA

WATU watatu wameuawa wawili kati yao wakiwa wanajeshi.

Tukio hilo la shambulizi la bomu lililotokea kwenye msafara wa jeshi Mogadishu, mji mkuu wa Somalia.

Ilitangazwa kuwa shambulizi hilo lililenga ofisa mkuu wa jeshi.

Iliripotiwa kuwa ofisa huyo alisema alinusurika tukio hilo bila kujeruhiwa, lakini wanajeshi wawili na raia mmoja, walifariki katika mlipuko huo.

Hakuna mtu aliyekamatwa kwa madai ya kuhusika na shambulizi hilo. **TRT**



Waandamanaji wakipiga kelele katika vizuizi walivyoweka wakati wa maandamano dhidi ya mapinduzi ya kijeshi Yangon, Myanmar, jana. Polisi walifyatua gesi ya kutoa machozi na mabomu ya maji na kulikuwa na ripoti za risasi. **PICHA: AP**

# Myanmar yamfuta kazi balozi wa UN

**Naypyidaw,** MYANMAR

JESHI la Myanmar limemfuta kazi balozi wake katika Umoja wa Mataifa (UN), kwa madai ya kutoa shutuma za kuondolewa madarakani kwa kiongozi wa kiraia Aung San Suu Kyi.

Aidha, polisi wameendelea kuongeza ukandamizaji dhidi ya waandamanaji, kufuatia maandamano katika miji mikubwa ya nchini humo takribani mwezi.

Balozi Kyaw Moe Tun anadaiwa kuwa alivunja maelekezo ya serikali baada ya kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua kali na za haraka katika kurejesha demokrasia nchini Myanmar.

Kuondolewa kwake kunafuatia siku moja ya ukandamizaji na kukamatwa kwa waandamanaji kulikofanywa na vikosi vya usalama vya Myanmar, wakati nchi hiyo ikiingia wiki yake ya nne ya maandamano ya kila siku dhidi ya utawala wa kijeshi.

Ghasia zilizuka juzi kwenye mji wa kibiashara Yangon, wakati polisi walipozuia mapema maandamano ya amani na kufyatua risasi za mipira kutawanya raia.

Zaidi ya watu 770 wamekamatwa, kushitakiwa na kuhukumiwa tangu nchi hiyo itumbukie katika mgogoro.

Duru kutoka kwa mwanasiasa na daktari mmoja nchini Myanmar zilisema polisi waliwafyatulia risasi waandamanaji wanaopinga utawala wa kijeshi na kuwauwa watu wanne huku wengine wakijeruhiwa katika siku ya pili ya kamata kamata dhidi ya waandamanaji.

Mwanamke mmoja pia ameripotiwa kuuawa wakati polisi walipojaribu kuvunja maandamano ya walimu kwa kutumia mabomu ya kutoa machozi mjini Yangon.

Sababu hasa ya kifo chake bado haijajulikana.

Mnyamnar imekuwa katika machafuko tangu jeshi lichukue nchi. **DW**

## HABARI MICHEZO



# GERRARD SASA ATAJWA LIVER KUMRITHI KLOPP

**LIVERPOOL,** England

STEVEN Gerrard anaweza kurudi haraka pale Anfield, kama kocha wa kuinoa Liverpool akichukuwa nafasi ya Jurgen Klopp, kwa mujibu wa gazeti la The Mirror.

Klopp alimaliza kipindi cha ukame wa miaka 30 wa Liverpool na kutwaa taji la Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza kwa kipindi hicho msimu uliopita, lakini raia huyo wa Ujerumani inaonekana anakaribia kurudi nyumbani kwao.

Liverpool haijawa na matokeo mazuri katika miezi ya hivi karibuni na kuibua uvumi kwamba Klopp anaweza kutupiwa virago wakati wowote.

Vijogoo hao wa dimba la Anfield kwa sasa wanapambana kuhakikisha angalau wanamaliza ligi wakiwa kwenye nne bora, kwani wapo nafasi ya sita katika msimamo.

Na iwapo Klopp ataondoka, ni wazi kwamba, Gerrard atarudi kwenye kikosi hicho kuchukuwa mikoba ya ukocha.

Liverpool imeripoti kwamba, wanatarajia Klopp akachukua nafasi ya kuinoa timu ya Taifa ya Ujerumani, kuchukuwa nafasi ya kocha wa muda mrefu wa kikosi hicho, Joachim Low.

Gwiji wa Liverpool, Gerrard ndiye anayetajwa zaidi kuchukuwa nafasi ya Klopp baada ya kuwa na mafanikio katika klabu ya Rangers nchini Scotland.

Gerrard, ambaye amecheza zaidi ya mara 700 kwa Liverpool, alichukuwa mikoba ya kuinoa Rangers mwaka 2018.

# Conte: Kuinoa Inter Milan ni kazi ngumu

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amebainisha kwamba, kuinoa Inter Milan ndio changamoto yake kubwa zaidi katika maisha yake ya ukocha.

Inter inapambana na AC Milan kuwania taji lake la kwanza la Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa kipindi cha muongo mmoja sasa.

Kabla ya mchezo wa jana, Jumapili dhidi ya Genoa, Inter walikuwa kileleni mwa msimamo wa Serie A baada ya mechi 23 wakiwa wanaongoza kwa tofauti ya pointi nne dhidi ya wapinzani wao Milan.

Inter ambao walimaliza nafasi ya pili kwenye Ligi ya Serie A nyuma ya Juventus kwa tofauti ya pointi moja, ukiwa msimu wa kwanza wa Conte kuinoa kwa mara ya mwisho walishinda taji hilo msimu wa 2010-11.

Lakini sasa Conte ameibuka na kusema kwamba, katika maisha yake ya ukocha, kuinoa Inter ndio changamoto yake kubwa zaidi kisoka.

“Wakati watu wanapozungumza kuhusu mimi, mara zote wanasema: ‘Yeye ni kocha mzuri, lakini hilo linanipa presha kubwa mimi,” alisema Conte akiiambia d Il Corriere Della Sera.

“Hii ni tofauti na sehemu nyingine, kwa sababu watu wanakuwa na matarajio makubwa sana na wewe, hivyo najikuta kwenye wakati mgumu sana.”





# *Tuchel afichua ya PSG na Fernandes*

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amebainisha kwamba, Paris Saint-Germain ilijaribu kumsajili Bruno Fernandes kabla hajajiunga na Manchester United mwaka jana.

Akizungumza kabla ya mchezo wa jana Jumapili ambao Chelsea ilikuwa ikiivaa Man United kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Tuchel ameelezea kwamba, wakati wa kipindi chake akiwa kocha mkuu wa PSG kutoka mwaka 2018 hadi 2020, mabingwa hao wa Ligue 1 walijaribu kumsajili Fernandes pale jijini Paris.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno wakati huo alikuwa nahodha wa Sporting CP, lakini alisajiliwa United Januari 2020 na tangu hapo amefunga jumla ya mabao 34 katika mechi 60 alizocheza kwenye mashindano yote.

“Nikiwa na Mkurugenzi wa Michezo wa kwanza pale Paris, Antero Henrique raia wa Ureno, alikuwa anamjua vizuri sana Fernandes,” alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

“Tulipambana sana kutaka kumleta kwenye timu yetu. Tulijaribu kwa nguvu zote, lakini hatukufanikiwa.

# Jina la Messi latawala wagombea urais Barca

**BARCELONA,** Hispania

WAKATI joto la uchaguzi wa urais ndani ya Klabu ya Barcelona linaendelea kufukuta, kila mgombea amezungumzia lake juu ya hatma ya Lionel Messi.

Uchaguzi unatarajiwa kufanyika Machi 8, mwaka huu, huku wagombea wa nafasi hiyo wakiwa watatu, Joan Laporta, Victor Font na Toni Freixa.

Laporta alishawahi kuwa Rais wa Barcelona kati ya mwaka 2003 na 2010 na ndiye anayepigiwa upatu zaidi kuipata nafasi hiyo.

Wagombea hawa wakiwa kwenye mahojiano ya pamoja na na Kituo cha Televisheni cha TV3, wote kwa pamoja walibainisha kuwa na nia ya kutaka kuweka mkakati wa kuibakiza huduma ya Messi klabuni hapo.

Kila mmoja alipata nafasi ya kutuma ujumbe kwa messi kupitia sanamu ambayo ilikuwa imevishwa jezi namba 10, anayovaa Messi.

Laporta aliikumbatia na kuibusu sanamu hiyo akasema kuwa atampatia ofa ambayo Messi hawezi kuikataa.

Hata hivyo, licha ya Freixa na Font pia kubainisha kuwa wangejaribu kumshawishi Messi kusalia klabuni hapo, bado wamesema kuwa chochote kinachoweza kutokea wanamshukuru kwa huduma yake na mapenzi yake yaliyotukuka kwa Barcelona.





# UNITED WAFIKIRIA KUMUUZA MARTIAL

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuwa ipo tayari kufikiria uwezekano wa kumuuza Anthony Martial wakati wa usajili wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alikuwa na msimu mzuri kwa msimu wa 2019-20 akiwa na 'Mashetani Wekundu' hao, akicheka na nyavu mara 23 katika mechi 48 kwenye mashindano yote, sambamba na usaidizi wa mabao 12.

Kwa mujibu wa Eurosport, United bado wanania ya kumsajili Jadon Sancho wa Borussia Dortmund na wanaweza kumruhusu Martial kuondoka kama mchezaji huyo wa kimataifa wa England ataafikiana na hilo.

Ripoti hiyo inadai kwamba wahusika wakuu huko Old Trafford watakuwa tayari kuzingatia "ofa kubwa" kwa Mfaransa huyo kutokana na hali yake katika msimu huu.

Martial, aliyefunga mabao 78 katika mechi 254 za Mashetani Wekundu za mashindano yote, ana mkataba na kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer hadi Juni 2024.

# *Martinez kuongeza mkataba Inter Milan*

**MILAN,** Italia

LAUTARO Martinez yuko tayari kusaini mkataba mpya na Inter Milan, na amesema mpango wa kwenda Barcelona ulikuwa zamani.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 23, alikuwa na hamu kubwa kutimkia Barcelona mwaka jana wakati klabu hiyo ilipokuwa ikijiandaa na kuondoka kwa Luis Suarez.

Suarez aliondoka kwenda Atletico Madrid wakati Barca ilipokabiliwa na shida za kifedha, hivyo kubaki na Lionel Messi, Antoine Griezmann na Martin Braithwaite kama chaguzi lao kuu kwenye safu ya ushambuliaji.

"Ni kweli, nilikuwa kwenye mazungumzo na Barcelona," alisema Martinez akiliambia Gazzetta dello Sport.

"Nilikuwa wazi na Antonio Conte, nilimwambia: 'Ninafikiria tu juu ya Inter, hii haitaniathiri'.

"Lakini, yote ni ya zamani. Nitaenda kusaini nyongeza ya mkataba na Inter."

Tangu ajiunge na klabu hiyo mwaka 2018, Martinez ameibuka kama mmoja wa washambuliaji wakali kwenye mchezo huo.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KOEMAN AFUNGUKA SABABU GRIEZMANN KUISHIA BENCHI

Tuliamua kubadilisha mfumo ili kujaribu kupata matokeo na tukamuweka mbele Dembele...

**SEVILLE,** Hispania

RONALD Koeman amesisitiza hakuwa na nia ya kutuma ujumbe kwa Antoine Griezmann kuwa amempa adhabu, kwa kumuacha benchi mshambuliaji huyo wakati Barcelona ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Sevilla.

**Griezmann amecheza mechi sita bila bao katika mashindano yote na aliwekwa kwenye wachezaji wa akiba wa Barca katika mchezo huo wa juzi, Jumamosi.**

Tofauti na mchezo wa ushindi wa 3-0 dhidi ya Elche katikati ya wiki, raia huyo wa Ufaransa hakuingizwa kucheza na badala yake Martin Braithwaite aliingizwa wakati wakiwa mbele kwa bao 1-0.

Akielezea uamuzi wa kumuingiza Braithwaite badala ya Griezmann katika dakika za mwisho, Koeman alisema: "Si ujumbe, hapana.

"Tuliamua kubadilisha mfumo na ili kujaribu kupata matokeo na tukamuweka mbele Dembele.

"Baada ya bao la kwanza, tulisema tunahitaji mtu mwenye kasi kuliko Griezmann kwa upande wa (Lionel) Messi. Na haikuwa adhabu."

Kwenye mchezo huo, Messi alifunga mabao yote mawili katika dimba hilo la Ramon Sanchez-Pizjuan, huku la kwanza pasi ya mwisho ikitoka kwa Dembele.

Huo ulikuwa ushindi wa tisa kwa Barca katika mechi 10 za LaLiga ugenini na kuwaacha wakipitwa ponti mbili na vinara Atletico Madrid, ambao wana mechi kadhaa mkononi.

Miamba hao wa Catalunya watakumbana tena na Sevilla Jumatano pale Camp Nou, kwenye mchezo wa pili wa nusu fainali ya Kombe la Mfalme (Copa del Rey).

Katika mchezo wa kwanza, Barcelona walichezea kichapo cha mabao 2-0, hivyo wana kazi ya ziada kupindua matokeo hayo.

## ZISIKUPITE

### BARNES KUONGEZA MKATABA

LEICESTER City imefikia pazuri kuhusu mazungumzo ya kumuongezea mkataba kiungo wake, Harvey Barnes, mwenye umri wa miaka 23, ambaye amekuwa anawindwa na Liverpool na Manchester United. ***(Sunday Mirror)***

### CAVANI KUIGHARIMU UNITED

MANCHESTER United watalazimika kumlipa straika wa kimataifa wa Uruguay, Edinson Cavani, pauni milioni 1.75 kama hawatamwongezea mkataba mchezaji huyo mwenye umri wamiaka 34. ***(Times)***

### MARTINEZ AITOSA BARCA

STRAIKA wa Argentina, Lautaro Martinez, 23, amesema alifanya mazungumzo na Barcelona, lakini ilikuwa zamani na sasa anatarajia kuongeza mkataba na Inter Milan. ***(Gazzetta dello Sport, via Goal)***

### PSG ILIMTAKA BRUNO

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesema walijaribu kumsajili kiungo wa Manchester United na Ureno, Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 26, wakati akiwa kocha wa Paris St-Germain. ***(Metro)***

### NEUHAUS HANA WASIWASI

KIUNGO wa Borussia Monchengladbach, Florian Neuhaus, 23, amesema hana wasiwasi kuhusu majaliwa yake, licha ya kuhusishwa na klabu za Ligi Kuu England, Tottenham na Liverpool. ***(football.london)***

### VARANE NA MKATABA MPYA

REAL Madrid itatoa ofa kwa mlinzi wa Ufaransa, Raphael Varane, 27, kipindi cha majira ya joto ili kumwongezea mkataba wake unaomalizika mwaka 2022. ***(AS, via Mail on Sunday)***

### WAKOMAA NA ODERGAARD

REAL Madrid inaamini kiungo wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 22, Martin Odergaard, ambaye anacheza kwa mkopo kule Arsenal, ana nafasi kubwa kwa baadaye kwenye kikosi chao. ***(Marca)***

### EVERTON YAMUWANIA SIMA

EVERTON inamfuatilia mshambuliaji wa Everton na Senegal, Abdallah Sima, 19, ambaye anaichezea Slavia Prague. ***(Football Insider)***

### JOSEPH AWINDWA

ARSENAL, Celtic na Rangers ni miongoni mwa klabu zinazowania kumsajili straika wa Wigan na Scotland, Kyle Joseph, 19, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(Sunday Mirror)***

### CARTER-VICKERS KUTOSWA

KLABU ya Tottenham Hotspur haina mpango wa kumpa ofa ya mkataba mpya mlinzi wake wa kati raia wa Marekani, Cameron Carter-Vickers, 23, ambaye anacheza kwa mkopo kule Bournemouth. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

# Ngome FC matumaini kibao kupanda Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Ngome FC imesema licha ya kupoteza michezo mitatu na kutoka sare tatu katika mzunguko wa Kwanza wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, bado inamatuimaini makubwa ya kupanda Ligi Kuu msimu ujao.

Ngome FC imemaliza mzunguko wa kwanza ikiwa nafasi ya tatu na alama 18 huku ikishinda michezo mitano katika ya 11 iliyocheza hadi sasa.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Kocha wa timu hiyo, Suleiman Mohmed Suleiman "Mo", alisema timu yake imejiandaa vema kuukabili mzunguko wa pili wa ligi hiyo huku matarajio yao makubwa yakiwa kupanda Ligi Kuu.

Alisema kupoteza michezo miwili ya mwisho ya mzunguko wa kwanza, haimaanishi kuwa safari yao ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao ndio imeishia hapo.

"Mzunguko wa kwanza tumecheza vizuri mpaka na tuliongoza ligi kwa muda wa wiki moja, na hata anayeongoza kwa sasa ligi hiyo, hatukupishana naye alama nyingi ambazo zinaweza kutufanya kupoteza matumaini ya kupanda Ligi Kuu, bado malengo yetu yapo palepale," alisema.

Aidha, alisema michezo waliyopoteza ilikuwa na upinzani mkubwa na migumu kwa kuwa ilikuwa dhidi ya timu ambazo zipo katika hatari ya kushuka na zile zilizopo juu katika msimamo wa ligi hiyo.

Ngome FC juzi ilijikuta ikiambulia kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya timu ya Kilimani City kwenye mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Mau B, wakati kwenye dimba Amaan timu ya Jang'ombe Boys na Mwembe Makumbi City zikitoka suluhu.

Mzunguko wa lala salama wa ligi hiyo unatarajiwa kuendela Machi 2, Kisiwani Unguja.

# KOCHA KEN GOLD ATOA SABABU KICHAPO YANGA

**Na Adam Fungamwangoo**

KOCHA Mkuu wa Ken Gold ambayo ilifungwa bao 1-0 Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Salvatory Edward, amesema wachezaji wake walicheza kwa kutojiamini wakihofia majina makubwa ya wachezaji wa Yanga.

**Akizungumza baada ya mechi hiyo, Salvatory, kiungo wa zamani wa Yanga, alisema kama isingekuwa hivyo, anafikiri hali ingekuwa tofauti kwenye mechi hiyo ya Kombe la FA.**

"Matokeo ndiyo kama hayo. Tumefungwa kwa sababu ya kutojiamini kwa wachezaji wangu, hilo ndilo limetuangusha. Kama wangetulia na kutoogopa majina ya wachezaji wa Yanga, mechi hii ingekuwa tofauti," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, alisema baada ya kutolewa kwenye michuano hiyo, akili yao wanaielekeza kwenye Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

"Ni mechi ambayo imetuongezea kitu. Wachezaji wangu wamecheza na wachezaji wakubwa, naamini itawaongezea ari ya uwezo wa kujiamini kwenye ligi yetu tunayoendelea nayo.

Timu hiyo, ipo Daraja la Kwanza Tanzania Bara, Kundi A, ikipigana kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, ikiwa inashika nafasi tatu kwa pointi 16, ikicheza michezo 10 mpaka sasa.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, alisema mechi ilikuwa ngumu upande wao kwa sababu walicheza na timu yenye uwezo mkubwa wa kuchezea mpira, lakini pia wachezaji wenye miili mikubwa.

"Ni timu ambayo imetupa upinzani sana. Kwanza ina wachezaji wenye miili mikubwa, halafu wamezoea kuchezea mpira, lakini kitu kikubwa hapa tumeshinda mechi," alisema.

Likuwa ni bao la Fiston Abdulrazack alilofunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 42, likitosha kuipa ushindi Yanga na kusogeza hatua ya 16 bora ambapo sasa itakutana na KMC FC.

NAMBA MOJA...



Mshindi wa kwanza mbio za Kilomita 42 za Kilimanjaro Marathon kwa upande wa wanawake, Jackline Juma, akimaliza mbio hizo zilizofanyika mjini Moshi mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dube awasha moto Azam ikiifuata Polisi FA

**Na Mwandishi Wetu**

BAO pekee la mshambuliaji Mzimbabwe Prince Dube dhidi ya Mbuni FC, limeipeleka Azam FC hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) maarufu FA Cup, ambapo sasa itakutana na Polisi Tanzania.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam juzi, Dube aliiandikia timu yake bao hilo katika dakika ya 45 ya kipindi cha kwanza, ambalo lilidumu hadi mchezo unamalizika.

Kwa ushindi huo wa Azam FC inayonolewa na Kocha Mkuu, Mzambia George Lwandamina, unaifanya kuungana na Kagera Sugar, Simba, Yanga, KMC FC, Polisi Tanzania ambazo tayari zimetinga hatua ya 16-bora.

Mchezo wake wa raundi ya tano sasa Azam FC itakutana na Polisi Tanzania inayonolewa na Kocha Mkuu, Hamsini Malale, katika Uwanja wa Azam Complex.

Tayari Azam FC imeweka wazi kwamba malengo yake makubwa ni kupata ushindi kwenye mechi zao zilizobaki ili kuwania tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

Ofisa Habari wa Azam FC, Zakaria Thabit 'Zaka Zakazi', alimwambia mwandishi wetu kuwa malengo yao ni kuona wanapata matokeo chanya kwenye mechi zao ambazo watacheza na kuweza kutwaa mataji.

Bingwa wa michuano hiyo ya FA Cup ataiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, ambayo kwa sasa Namungo FC inaendelea kuipeperusha bendera ya Tanzania msimu huu baada ya kufuzu hatua ya makundi.

Azam inayoshika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 37 baada ya mechi 21, bado ipo kwenye mbio za kuwani taji hilo ambalo bingwa huiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Jumatano Azam itashuka katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba kuivaa Kagera Sugar katika mwendelezo wa mbio zao za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Bara, wakati huu Yanga yenye pointi 49 baada ya mechi 21 ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikifuatiwa na Simba yenye alama 42 na mechi tatu mkononi.

# Michezo

Jumatatu Machi 1, 2021

Nipashe




Koeman afunguka sababu Griezmann kuishia benchi UKURASA 22

MEDALI...



Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Abdallah Ulega, akimvisha medali mshindi wa kwanza wa mbio za Kilimanjaro Marathon Kilomita 42 kwa upande wa wanaume, Abel Chibet, zilizofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro jana, nyuma yake ni Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Irene Mutiganzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba kuitafutia kasi Al-Merrikh kwa JKT leo

## Gomes asema hesabu zote Ligi Kuu kwanza kabla ya kesho kukwea pipa kuwafuata Wasudan hao huku...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya juzi kutinga hatua ya 16-bora ya Kombe la Azam Federation maarufu FA Cup, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, leo watashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha JKT Tanzania katika kinyang'anyiro cha ligi hiyo, huku wakitumia mchezo huo kujiandaa na mechi ijayo dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan.

**Simba ambayo Ijumaa iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya African Lyon kwenye mechi hiyo ya Kombe la FA, kesho itapanda ndege kuifuata Al-Merrikh kwenye mechi yao ya tatu ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara, wataifuata Al-Merrikh wakiwa tayari wameshinda michezo yao miwili baada ya kuichapa AS Vita ya DR Congo bao 1-0 ikiwa kwao kabla ya Jumanne iliyopita kuibuka na ushindi kama huo hapa nyumbani dhidi ya Al-Ahly ya Misri.

Simba ambayo pia ni bingwa mtetezi wa Kombe la FA, sasa itakutana na Kagera Sugar katika mechi ya raundi ya 16-bora.

Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes amesema, hesabu zao kwa sasa ni mechi dhidi ya JKT Tanzania kwa kuwa malengo yao kwanza ni kutwaa mataji yote mawili, Kombe la FA na ubingwa wa Ligi Kuu, huku wakifanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Gomes alimwambia mwandishi wetu kuwa katika mchezo huo wa leo dhidi ya JKT Tanzania, ataendelea kufanya mabadiliko ya kikosi chake ili kutoa mapumziko kwa baadhi ya nyota wake.

Alisema ana imani kubwa na kikosi chake na kwamba wachezaji watakaopata nafasi wanaweza kupambania timu kupata matokeo chanya.

"Kwa ujumla ligi imekuwa na ushindani mkubwa, lakini kwetu sisi malengo yetu ni kila mechi kupata matokeo chanya, kwa sasa tunasahau matokeo ya mechi iliyopita na kuelekeza akili yetu kutafuta pointi tatu dhidi ya JKT Tanzania.

"Tunajua ni mechi ngumu kwa kuwa tunahitaji kupata pointi muhimu ili kujiweka katika mazingira mazuri kwenye mbio za ubingwa, lakini tutapambana," alisema Gomes.

Kuhusu kurejea kwa John Bocco alisema: "Hakuwa majeruhi, alikuwa anaumwa maradhi ya kawaida na sasa amerejea, hivyo tunahitaji huduma yake."

Simba itashuka dimbani leo ikiwa na matumaini makubwa ya kuendeleza ushindi wao wa Oktoba 4, mwaka jana dhidi ya JKT Tanzania baada ya kuwachapa wanajeshi hao mabao 4-0 katika mzunguko wa kwanza kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma wakati wakinolewa na Kocha Mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

Mabao ya Simba katika mechi hiyo yalifungwa na Meddie Kagere aliyetupia mawili dakika ya nne na 40 na mengine yakifungwa na Chris Mugalu dakika ya sita na Luis Miquissone akihitimisha ushindi huo dakika ya 51.

# Kaze alia majeruhi akiisifu Ken Gold

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema kuwapo kwa majeruhi na kukosa wachezaji imara kikosini huku wapinzani wao Ken Gold wakimudu kuuchezea vema mpira, ni moja ya sababu ya kulazimika kucheza mchezo wa nguvu zaidi.

Akizungumza na gazeti hili jijini juzi, Kaze alisema kwa sasa kikosi chake kimeandamwa na majeruhi hali inayoendelea kuitesa timu yake na kushindwa kucheza kwa kiwango walichokionyesha mzunguko wa kwanza.

Alisema suala la kupata wachezaji wazuri lilifanyiwa kazi kwa asilimia ndogo kwa sababu kipindi cha usajili wa dirisha dogo walifanyia kazi katika nafasi chache.

"Tulifanya usajili lakini hatuwezi kuacha wachezaji nane kwa kusajili wengine, hivyo tukaongeza nafasi muhimu ikiwa ni pamoja na safu ya ushambuliaji, tunapokuwa na majeruhi kama sasa tunashindwa kupata mbadala wa kuziba nafasi zao.

"Nina imani kuna baadhi ya majeruhi wameanza kupona, mechi zijazo watakuwa fiti na kusaidia timu kupata matokeo chanya," alisema Kaze ambaye kikosi chake Alhamisi kitashuka Uwanja wa Mkwakwani mkoani Tanga kuwavaa wenyeji Coastal Union kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara.

Kuhusu timu yake kushinda kwa mkwaju wa penalti kwenye Kombe la FA dhidi ya Ken Gold, Kaze, alisema mechi ilikuwa ngumu upande wao kwa sababu walicheza na timu yenye uwezo mkubwa wa kuchezea mpira, lakini pia wachezaji wenye miili mikubwa, lakini kikubwa wametinga hatua ya 16-bora.

"Ni timu ambayo imetupa upinzani sana. Kwanza ina wachezaji wenye miili mikubwa, halafu wamezoea kuuchezea mpira, lakini kitu kikubwa hapa tumeshinda mechi," alisema

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >